BILL PINTO

# Yesu Mwingine, Injili Nyingine

NA MAJIBU YA VIPINGAMIZI



## HOFU YA UONGO

> 2 Wakorintho 11:3 **Lakini nachelea**; kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asije **akawaharibu fikira zenu, mkauacha unyofu na usafi wa Kristo**.

Kwenye barua zake kwa Wakorintho, mtume Paulo anaitaja injili pekee ya kweli, akiiita "usahili ulio ndani ya Kristo". Japokuwa pamoja na maagizo haya, Paulo aliogopa kuwa wengine wangejaribu kuupinga kweli alioufundisha ambao unaeleweka kirahisi, na hivyo akawashauri wanaoamini wasimkubali Yesu mwingine na injili nyingine:

> 2 Wakorintho 11:4 Maana yeye ajaye akihubiri Yesu mwingine ambaye sisi hatukumhubiri, au mkipokea roho nyingine msiyo ipokea, au injili nyingine msiyoikubali, **mnatenda vema kuvumiliana naye!**

Paulo alikuwa na wasiwasi kuwa baada ya kuwashirikisha wengine ukweli ambao unaeleweka kirahisi kuhusu Mungu na Mwanawe, wengine wangekuja kuishirikisha injili ya uongo, wakihubiri kuhusu Yesu mwingine na Roho Mtakatifu mwingine. Zaidi ya hayo, Paulo alitabiri kuwa kanisa "linaweza kumvumilia [au kumkubali] yeye [mwalimu wa uongo]"!

Cha kusikitisha ni kuwa hofu ya Paulo imekuwa ni kweli. Leo hii idadi kubwa ya makanisa ya Kikristo humtangaza mungu wa utatu. Injili nyingine imeingia.

Ninakusihi usidanganywe kwa kufikiri kuwa hili ni jambo dogo. Ama ujumbe uliomo ndani ya kitabu hiki ni injili ya uongo, au fundisho la utatu ni ya kweli. Hakika, imani hizi mbili zisingeweza kuwa mbali zaidi kutoka kwenye kila moja wapo. Kama utakavyogundua hivi karibuni, fundisho moja limeegemea juu ya vifungu vya Maandiko yaliyo wazi tu, wakati fundisho lingine limejengwa juu ya dhana na nadharia za kubahatisha.

Enyi marafiki, jifunzeni kwa uangalifu. Hakuna msingi wowote wa katikati.

## MAFUMBO NA MAJUKUMU YA KILA MMOJA

> Imani Namba 2 ya Msingi wa Kanisa la Waadventista
> Utatu: Kuna Mungu Mmoja: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, umoja wa Nafsi tatu za milele...

Hakuna mstari hata mmoja kwenye Biblia ambayo inafundisha kuwa Mungu ni muunganiko wa watu watatu wa milele. Kinyume chake, Biblia inatangaza hivi:

> Kumbukumbu la Torati 6:4 Sikiza, Ee Israeli; BWANA Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja.

Angalia namna inavyofurahisha, wakati fulani Yesu aliulizwa hivi na mwandishi: “Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza?” (Marko 12:28). Kama ilivyokuwa desturi yake, Bwana alijibu kwa kunukuu Maandiko ya Agano la Kale. Lakini ona ni kifungu gani ambacho Yesu anarejelea kwenye kujibu swali hili:

> Marko 12:29 Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja;

Kwenye kujibu swali, "amri ya kwanza katika zote ni ipi?" Yesu anakumbuka Kumbukumbu la Torati 6:4, akikazia umuhimu wa kumuamini Mungu mmoja. Kwenye barua yake kwa Wakorintho, mtume Paulo anaelezea waziwazi Mungu huyo mmoja ni nani:

> 1 Wakorintho 8:6 Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake...

Paulo anasema wazi wazi kuwa kuna “Mungu mmoja, Baba”. Hii inarudiwa kwenye barua yake kwa Waefeso, ambapo anasema hivi:

> Waefeso 4:6 Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.

Pia, Yakobo anaandika akisema hivi:

> Yakobo 2:19 Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema...

Hatimaye, tunasoma maneno ya Yesu Mwenyewe:

> Yohana 17:3 Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.

Kwa kuzilinganisha Yohana 17:3 na Marko 12:29, inakuwa ni wazi sana kuwa Yesu alipoinukuu Shema ya Israeli ("Sikia, Ee Israeli; Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja"), alikuwa akimaanisha Baba Yake; "Mungu wa pekee wa kweli".

Baba ndiye chanzo cha uzima wa watu wote, pamoja na uzima wa Mwanawe (Yohana 5:26). Hii ndiyo sababu Yesu anaitwa "Mwana pekee wa Mungu" (Yohana 3:18). Kwa asili, Yeye ni sawa na Mungu. Na Biblia inatuambia kuwa Baba aliviumba vitu vyote kwa Mwana wake (Waefeso 3:9, Waebrania 1:2). Zaidi ya hayo, Biblia inaeleza mara kwa mara kuwa Roho Mtakatifu ni uwepo binafsi wa Baba na Mwana. (Warumi 8:9, Wagalatia 4:6, Yohana 20:22, Yohana 14:23.) Ni Roho wao, na si kiumbe wa tatu wa ajabu.

Licha ya kauli hizi, Gordon Jensen—mwanatheolojia mkuu kutoka kwenye Chuo Kikuu cha Andrews—anaandika hivi:

> Mpango wa wokovu ulizungukwa kwenye agano lililofanywa na Nafsi Tatu za Uungu, ambazo kwa usawa zilikuwa na sifa za Uungu. Ili kuondoa dhambi na uasi kutoka kwenye ulimwengu na kurejesha upatanisho na amani, mmoja wa Viumbe wa Kimungu alikubali, na aliingia kwenye jukumu la Baba, jukumu lingine la Mwana…

Maneno ya Jensen yanaashiria mafundisho ya kiorthodoksi ya Kanisa la Waadventista Wasabato. Na kupitia taarifa hii pekee, Jensen na Kanisa la Waadventista wanasema kuwa hakuna Baba na Mwana. Badala yake, wanapendekeza kuwa "mmoja wa Viumbe wa Uungu alikubali, na aliingia kwenye jukumu la Baba, mwingine jukumu la Mwana".

La zaidi, ni kuwa kwenye andiko la *Understanding the Trinity* la Mchungaji Max Hatton, tunasoma hivi:

> Uhusiano wa Baba na Mwana kwenye Uungu unapaswa kueleweka kwenye maana ya mafumbo/sitiari, si kwenye maana halisi.

Sitiari ni ishara, tamathali ya usemi, taswira au mafumbo. Kwa asili, siyo kweli. Kwani mara unapofundisha watu watatu wa milele, hauwezi kumuamini Baba na Mwana halisi. Ni kwa sababu hii kuwa Kanisa la SDA linafundisha kuwa uhusiano wa Baba na Mwana ni kwenye majukumu ya kila mmoja; ni kwenye "kueleweka kwa maana ya mafumbo/sitiari" tu.

Hata hivyo, kwenye kushikilia fundisho hili, wanaoamini kwenye utatu wanalazimika kuvikataa vifungu vya Maandiko vilivyo wazi vilivyonenwa na Kristo Mwenyewe, na hata vile vilivyonenwa na Baba aliye mbinguni. Na kwa kukataa kwao injili hii ambayo ni rahisi, wanalazimika kuitambulisha injili nyingine.

Tafadhali pitia kauli zilizotajwa hapo juu zilizotolewa na viongozi wa kanisa la Waadventista. Hakuna ushahidi wa kimaandiko unaotolewa. Mtu anapotoa kauli za aina hizi—ambazo zinasambazwa ulimwenguni pote—ni lazima uungaji mkono thabiti wa kimaandiko uoneshwe, na kile ambacho hakipingani na Maandiko mengine!

Tazama ushauri wa hekima tunaopewa kwenye kitabu cha Ellen White kiitwacho *The Great Controversy*:

> Habari za kweli zilizofunuliwa kwa uwazi zaidi kwenye Biblia zimehusika kuwapa mashaka na giza watu wasomi, ambao, kwa kujifanya kuwa na hekima kuu, wanafundisha kuwa Maandiko yana mafumbo, maana ya siri, ya kiroho isiyoonekana kwenye lugha inayotumika. Watu hawa ni walimu wa uongo…Lugha ya Biblia inapaswa kufafanuliwa kulingana na maana yake iliyo dhahiri, isipokuwa kama ishara au mfano umetumika…Kama watu wangeichukua Biblia kama inavyosomwa, kama kusingekuwa na

walimu wa uongo wa kuwapotosha na kuwavuruga akili basi kazi ingetimizwa ambayo ingewafurahisha malaika na ambayo ingewaingiza zizini mwa Kristo wale maelfu kwa maelfu ambao sasa wanatangatanga kwenye makosa. (GC 598)

Enyi marafiki, unapoambiwa kuwa uhusiano wa Baba na Mwana ni wa mafumbo, kuwa Yesu si Mwana kihalisi, na kuwa hana Baba halisi, kumbuka ni nani anayezungumza kwenye Yohana 3:16. Mara nyingi tunasahau kuwa haya ni maneno yenyewe ya Kristo, na kuwa hii ndiyo injili ambayo inapaswa kuvuka kila taifa, kabila, lugha na watu. Injili ambayo hata mtoto anaweza kuielewa! Hakika haumhitaji mwanatheolojia kukuambia maana ya "mwana wa pekee". Ni ukweli rahisi unaojieleza. Fikiria vifungu vifuatavyo vilivyo wazi kabisa:

> Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

> 1 Yohana 4:9 Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye.

Uthibitisho wa Biblia unasema kuwa kumjua Mungu ni kumpenda Yeye, na mtu humpenda Mungu kwa kuamini Yeye ni nani na kile ambacho Amewafanyia. Ewe rafiki, Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni ili kukuokoa. Siyo mtu anayechukua nafasi ya Mwana. Si mafumbo. Mwana wake wa pekee.

> Warumi 8:32 **Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe**, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?

Hizi zote ni kauli zilizo wazi. Si mafumbo, na wala si ishara fulani. Kwa kweli, Mungu alitaka kuliweka wazi sana kiasi kwamba alizungumza mara mbili kutoka mbinguni kuhusu jambo hili. Sauti ya Baba imeandikwa mara tatu tu kwenye Agano Jipya lote, na mara mbili ya maandiko hayo Yeye anashuhudia kuwa Yesu ni Mwanawe mpendwa. Angalia

maneno anayosema wakati wa ubatizo wa Kristo:

> Mathayo 3:17 na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, **Huyu ni Mwanangu**, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.

Sidhani kama watu hawatambui jinsi ambavyo si halali kumuita Mungu Baba na Mwanawe kuwa wanahusika kwenye mfano wa sitiari. Kumbuka, huyu ndiye Mungu Baba ambaye anazungumza. Je, tutasema kuwa maneno Yake hayapaswi kuchukuliwa kiuhalisia? Ni kwa namna gani tena mtu anapaswa kuielewa sauti kutoka mbinguni ikisema: "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu"? Tazama ni kwa namna gani ambapo Kristo alitukuzwa mbele ya Petro, Yakobo, na Yohana:

> Mathayo 17:5 Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, **Huyu ni Mwanangu**, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.

Tukiegemea kwenye kiini kikuu cha injili tunajua kuwa hii ni zawadi ya Baba kwa ajili ya wanadamu; zawadi ya Mwanawe pekee kama kipatanisho wa dhambi zetu. Lakini viongozi wa kanisa wanafundisha nini kuhusiana na ukweli huu ambao ni wa thamani?

> Uhusiano wa Baba na Mwana kwenye Uungu unapaswa kueleweka kwenye maana ya **mifuano**, si kwenye **maana halisi**.

Leo hii, wale wanaoamini kwenye utatu wanasema kuwa uhusiano wa Baba na Mwana ni wa sitiari. Kuwa hakuwa Mwana wa Mungu kiuhalisi ambaye alitumwa ili kufa. Na si Baba aliyemtuma kiuhalisi, bali ni yule ambaye "aliingia kwenye nafasi ya Baba, [na] mwingine ni kwenye jukumu la Mwana."

Kwa mafundisho haya, wanatheolojia wanadhoofisha dhabihu isiyo na kikomo ya Mungu na Mwanawe, na wanauficha upendo mkuu ambao Baba ameuonesha kwako na kwangu.

Zaidi ya hayo, fundisho la utatu linashindwa kutoa mstari mmoja

kama ushahidi wa Baba na Mwana wa mfanano huo wa sitiari/mfano. Hata hivyo, kila mmoja, Kristo, Baba, mitume, na Roho wa Unabii anaushuhudia ukweli huo huo: Baba na Mwana hawajaelezewa kimafumbo.

## KUFICHUA AU KUFICHA

> Shetani amedhamiria kwamba watu hawataona upendo wa Mungu ambao ulimpeleka kumtoa **Mwanawe wa pekee** ili kuokoa jamii iliyopotea... (Ellen G. White, Selected Messages Book 1, 156)

Shetani anatuzuiaje tusiuone upendo wa Mungu? Kupitia fundisho la utatu. Fundisho ambalo linatenganisha kiini cha injili na tumaini lenyewe la wokovu wa mwanadamu. Kwenye Yohana 3:36, tunaziona hali ambazo ni za wazi za kumfanya mtu apate uzima wa milele:

> Yohana 3:36 Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali adhabu ya Mungu inamkalia.

Kwa kudai kuwa Baba na Mwana ni maneno yenye sitiari, utatu unakana kuwa Yesu ni Mwana pekee wa Mungu. Kinyume chake, wokovu wetu unategemea sisi kuukubali ukweli huu!

> Yohana 3:18 Amwaminiye yeye hahukumiwi; **asiyeamini amekwisha kuhukumiwa**; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.

Hapa kuna changamoto. Ikiwa unaamini kuwa Mungu ni umoja wa nafsi tatu za milele, basi toa mstari mmoja wa Maandiko ili kuunga mkono ufafanuzi huu.

Kwa uhakika, hautapata maandiko hata ya sehemu moja. Wanatheolojia wanajua kuwa hakuna Maandiko ya kuyaunga mkono mafundisho yao. Hata hivyo, bado wanasisitiza kuwa uhusiano wa Baba na Mwana ni wenye msingi wa sitiari; kuwa ni suala la majukumu na uhusika tu.

Kinyume chake, Yesu anasema hivi:

> Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa **Mwanawe pekee**, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Baba anasema hivi:

> Mathayo 3:17 na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, **Huyu ni Mwanangu**, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.
>
> Mathayo 17:5 Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, **Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu**, ninayependezwa naye; msikieni yeye.

Mitume wanasema hivi:

> 1 Yohana 4:9 Katika hili pendo la Mungu lililoonekana kwetu, kwamba **Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni**, ili tupate uzima kwa yeye.
>
> Warumi 8:32 Yeye asiyemwachilia **Mwana wake mwenyewe**, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?

Ukweli kumhusu Mungu unaunganishwa kwa ustadi na jinsi Anavyowapenda wanadamu. Hata hivyo, kupitia fundisho la utatu, wahudumu wa Injili wanataka kumfanya Mungu kuwa ni mwongo:

> 1 Yohana 5:10 Yeye amwaminiye Mwana wa Mungu anao huo ushuhuda ndani yake. **Asiyemwamini Mungu amemfanya kuwa mwongo**, kwa kuwa **hakuuamini huo ushuhuda ambao Mungu alimshuhudia Mwanawe.**

Hivyo ndivyo Maandiko inatuhimiza tukubali ukweli huu mzuri. Kama hauamini "ushuhuda ambao Mungu alimshuhudia Mwanawe", unamfanya Mungu kuwa ni muongo. Bila shaka, tunajua kuwa Mungu hawezi kusema uongo. Basi, mbona ni vigumu sana kuamini maneno Yake yaliyo wazi na yenye upendo: **"na tazama, sauti kutoka mbinguni** ikisema, **Huyu ni Mwanangu**, mpendwa wangu, ninayependezwa naye."? (Mathayo 3:17).

Kwenye Mathayo 16:15, Yesu anawauliza wanafunzi wake swali la maana sana:

> "Akawaambia, **Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?**"

Kisha, akizungumza kwa niaba ya wale wanafunzi kumi na wawili, Petro anasema kuwa:

> "Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, **Mwana wa Mungu aliye hai.**
> Yesu akajibu, akamwambia, **Heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.**
> Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, **na juu ya mwamba huu** nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda"
> Mathayo 16:16-18.

Ona jinsi ambavyo Yesu anajibu maungamo ya Petero. Kuna mambo matatu muhimu ya kujifunza:

1. Yesu anambariki Petero kwa jibu alilitoa.
2. Yesu anasema kuwa ungamo la Petero ilifunuliwa kwake na Baba mwenyewe.
3. Yesu anasema kuwa ungamo la Petero ("Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai") ndiyo msingi wa kanisa la Kikris to.

Je, unaona jinsi ukweli huu ulivyokuwa ni wa muhimu sana? Yesu anasema kuwa kanisa lake limejengwa juu yake na "wala milango ya kuzimu haitalishinda". Ni kwa sababu hii kwamba utatu unaharibu msingi hasa wa kanisa la Mungu! Utatu unakana kuwa kweli Yesu ni Mwana wa Mungu, na kwa hiyo unakana maneno ya Baba, maungamo ya mitume, na ahadi za Yesu Kristo.

Kumbuka, wanaoamini kwenye utatu wanafundisha kuwa Mwana ni sitiari/fumbo tu. Kwa hiyo, kulingana na fundisho hili, kanisa zima la Kikristo limejengwa juu ya kitu ambacho si halisi. Inashangaza! Ukweli

mkuu zaidi kwenye Biblia—ukweli ulio imara sana kiasi kwamba Yesu anaitambua kama mwamba ambayo juu yake atalijenga kanisa lake—ni mfano au sitiara kulingana na wanaoendeleza imani ya utatu.

Kinyume chake, tazama jinsi mtume Petero alivyotilia mkazo umuhimu wa kutambua Yesu kuwa mwana wa Mungu. Kwenye 2 Petero 1, tunasoma wosia wa mwisho na ushuhuda wa mtume huyu aliyejiweka wakfu. Petro anapokaribia kufa, kuna jambo moja akilini mwake ambalo anataka watu wengine walikumbuke:

> 2 Petro 1:13 Nami naona ni haki, maadamu nipo mimi katika maskani hii, kuwaamsha kwa kuwakumbusha.
> 1:14 Nikijua kwamba kule kuwekea mbali maskani yangu kwaja upesi, kama Bwana wetu Yesu Kristo alivyonionyesha.
> 1:15 Walakini nitajitahidi, kwamba kila wakati baada ya kufariki kwangu mpate kuyakumbuka mambo hayo.
> 1:16 Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu zake Bwana wetu Kristo na kuja kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake.
> 1:17 **Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu, hapo alipoletewa sauti iliyotoka katika utukufu mkuu, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.**
> 1:18 **Na sauti hiyo sisi** tuliisikia ikitoka mbinguni tulipokuwa pamoja naye katika mlima ule mtakatifu.

Hapa tunaona imani ya Petero ilijengwa juu Yake. Kabla tu ya kifo chake, Petro anauweka bayana ukweli mmoja wa muhimu zaidi wa kushikiliwa na kanisa.

Fikiria juu yake: huyu ndiye mtume aliyetembea na Yesu tangu mwanzo wa huduma yake. Angeweza kuandika kuhusu miujiza ya Kristo, mafundisho Yake, uzoefu wa chumba kilicho juu, msalaba, ufufuo wake, au Pentekoste. Ila Petero ambaye ni mzee anapokaribia kufa anatuandikia ukweli wa maana sana wa huduma nzima ya Kristo. Kuwa yeye, pamoja na Yakobo na Yohana, walimuona Yesu akigeuka sura na kuisikia sauti ya Baba ikisema: “Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye”. Hakika, maneno ya mwisho ya Petro ni maungamo ya

dhati, ambayo kwa hayo anaongezea kusema hivi: "Na sauti hiyo sisi tuliisikia ikitoka mbinguni tulipokuwa pamoja naye katika mlima ule mtakatifu".

Enyi marafiki, utamuamini nani? Maneno ya Baba Mwenyewe? Au maneno ya wachungaji wanaomkana Baba na Mwana ambao ni halisi? Angalia ni nani amkanaye Baba na Mwana:

> 1 Yohana 2:22 Ni nani aliye mwongo ila yeye akanaye ya kuwa Yesu ni Kristo? **Huyo ndiye mpinga Kristo, yeye amkanaye Baba na Mwana.**

Yohana anathibitisha kuwa ni roho ya mpinga-Kristo inayekana Baba na Mwana. Inatoka Roma. Na Roma, kutoka huko Babeli.

Kwa wanaadventista, kuna imani kuu mbili kuhusu utatu:

1) Utatu: Imani ya Miungu 3 (tritheism)
2) Utatu: Mungu 1 kwenye nafsi 3 (Trinitarianism)

Imani zote mbili ni za uongo. Wote wanakana kuwa Yesu ni Mwana pekee wa Mungu. Na wote wanakana kuwa Roho Mtakatifu ni Roho binafsi ya Baba na Mwana. Imani ya pili—ambayo tunashughulika nayo—hakika ni fundisho la Kikatoliki la Roma. Kwenye Compendium of the Catechism of the Catholic Church tunasoma hivi:

> Nafsi **tatu** za Uungu ni Mungu mmoja tu...

Hivi ndivyo kanisa la SDA linavyotufundisha leo hii. Kwa hakika, Kanisa la Waadventista Wasabato na Kanisa Katoliki la Roma hufundisha:

- Mungu mmoja kwenye nafsi tatu.
- Watu watatu kwenye kiini kimoja.
- Tofauti ya watu.
- Watu wote watatu ni wa milele na ni sawa.
- Mungu huyu mmoja hawezi kugawanyika.
- Nafsi hizo tatu ni Mungu mmoja.

Enyi marafiki, Maandiko yametufundisha nini?

> 1 Yohana 2:22 ...Huyo ndiye mpinga Kristo, yeye amkanaye Baba na Mwana.

Kwa hakika inaweza kusemwa hivi:

> Waprotestanti wanaipoteza alama ya tofauti iliyowatofautisha na ulimwengu, na wanaupunguza umbali kati yao na mamlaka ya Kirumi. Wamegeuza masikio yao wasisikie yale yaliyo ya kweli; wamekuwa hawataki kukubali nuru ambayo Mungu aliwaangazia kwenye njia yao, na kwa hiyo wanaingia gizani. (Ellen G. White, Signs of the Times, Februari 19, mwaka 1894)

## BABA WA WOTE

> 1 Wakorintho 8:6 Lakini kwetu sisi **Mungu ni mmoja tu, aliye Baba,** ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yupo na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo.

Kwenye 1 Wakorintho 8:6, tunaiona kauli ambayo ni rahisi lakini ni ya ajabu. Hapa, mtume Paulo anasema kuwa kuna “Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake”. Kwa hakika Paulo hakuwa mtetezi wa 'mungu-mmoja-kwenye-watu-tatu'.

Zaidi ya hayo, kwenye Yohana 17:3, tunaonyeshwa maombi ya Kristo kwa ajili ya wanadamu. Uwe na uhakika, sala hii si ya ishara. Wala siyo ya mfano. Ni maneno ya Mwana kwenye ushirika na Baba yake:

> Yohana 17:3 **Na uzima wa milele ndio huu**, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.

Hapa, Yesu anataja ujumbe ule ule ambao Paulo anaushirikisha kwenye 1 Wakorintho 8:6. Na kwenye Waefeso 4:6, tunapata tena uwiano ufuatao:

> Waefeso 4:6 **Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote**, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.

Kwa hakika, kama vile Baba alivyo Mungu mmoja wa kweli, Yesu Kristo ndiye Mwanawe wa pekee. Kwenye Mithali 30:4, Sulemani anazitafakari kwa kina siku za uumbaji, na kuuliza hivi:

> Mithali 30:4 ... ni nani aliyefanya imara ncha zote za nchi? Jina lake ni nani? Na ni nani jina la mwanawe, kama wajua?

Hapa, mtu mwenye hekima zaidi aliyeishi anabainisha kuwa, Mwana wa Mungu alikuwa Mwana kabla ya uumbaji. Si Mwana tu akiwa kule Bethlehemu, lakini Mwana ambaye alikuwepo kabla ya Dunia kuumbwa. Na nabii Isaya anasema:

Isaya 9:6 Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa **mtoto mwanamume**;...

Unabii huu ni wa kitabu cha Yohana 3:16 cha Agano la Kale. Mtoto aliyezaliwa Bethlehemu ni Mwana ambaye aliletwa "kwetu". Mwana pekee wa Mungu.

Yohana 3:16 **Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee**...

3:17 Maana Mungu **hakumtuma** Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.

Ili Baba amtume Mwanawe ulimwenguni, Yesu alipaswa kuwa Mwana kabla ya Bethlehemu. Hiki hasa ndicho kinachoelezewa kwenye kifungu kifuatacho:

1 Yohana 4:9 Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba **Mungu amemtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni**, ili tupate uzima kwa yeye.

Kwa mara nyingine tena, tunaona kuwa Yesu alikuwa ni Mwana kabla kuzaliwa Bethlehemu, na Mwana huyo ndiye aliyetumwa kutoka mbinguni. Yohana pia asema hivi:

Yohana 1:14 ... nasi tukauona utukufu wake, **utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba**;...
Yohana 1:18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; **Mungu Mwana pekee** aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.

Leo hii, wengi wanakanusha ukweli kwenye aya hizi. Wanakataa kukubali kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu halisi. Kwa sababu hii, Mungu (kwenye rehema zake) analiweka wazi sana jambo hili:

Marko 15:39 Basi yule akida, aliyesimama hapo akimwelekea, alipoona ya kuwa alikata roho jinsi hii, akasema, **Hakika mtu huyu**

**alikuwa Mwana wa Mungu**.

Kufikia sasa, tumeona uwiano kamili kwenye Agano la Kale na Jipya kuwa Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee hapa ulimwenguni. Kisha, bila kuruhusu shaka yoyote, Maandiko yanasema hivi: "Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu"! Hata hivyo, ikiwa bado unakataa kuamini kwamba Yesu ni Mwana mzaliwa wa Mungu, zingatia kwa umakini maandiko ya Yohana 3:18:

> Yohana 3:18 Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu **hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu**.

Biblia inatuonya mara kwa mara kuwa uzima wetu wa milele unategemea sisi kumjua Baba na Mwana:

> Yohana 17:3 Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, **Mungu wa pekee wa kweli**, na Yesu Kristo uliyemtuma.

Fikiria tafsiri ya kamusi ya neno 'pekee':

> Pekee
> 1. Mmoja pekee yake; mmoja; kama, mtu pekee aliyepo; kazi yake pekee.
> 2. Pekee yake kwenye eneo lake; pekee yake; haihusiani na watu wengine wa tabaka moja au aina kama yake; kama, mtoto wa pekee.

Yesu anapomuita Baba "Mungu wa pekee wa kweli", anamaanisha kile anachokisema. Lakini makanisa ya Kiprotestanti na Katoliki yanasema kuwa Mungu ni wa asili ya nafsi tatu tofauti. Na kinyume chake, Paulo anasisitiza kuwa:

> 1 Wakorintho 8:6 Lakini kwetu sisi **Mungu ni mmoja tu**, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yupo na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo.

Baba ndiye Mungu wa pekee wa kweli kwa sababu Baba ndiye mwanzilishi wa vitu vyote. Yeye ndiye mtawala wa ulimwengu. Vitu vyote vilitoka kwa Mungu, ikimjumuisha Mwanawe. Kwa wakati huu, unaweza kuwa unajiuliza: Je, Yesu siyo muumba wetu? Hii ni kweli. Hata hivyo, angalia kwa umakini kile ambacho Paulo anafundisha:

> Waefeso 3:9 na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika **Mungu aliyeviumba vitu vyote kupitia mwana**;

> Waebrania 1:2 mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, **tena kwa yeye aliufanya ulimwengu**;

Ndiyo, Yesu aliviumba vitu vyote. Hiyo ni kweli. Lakini ukweli wa ndani zaidi ni kuwa Baba aliviumba vitu vyote kupitia Mwanawe. Zaidi ya hayo, kama Waebrania 1:2 inavyoonyesha, Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu wakati alipouumba ulimwengu! Hivyo ndivyo Sulemani anavyosema kwenye Mithali 30:4:

> Mithali 30:4 ... ni nani aliyefanya imara ncha zote za nchi? Jina lake ni nani? **Na ni nani jina la mwanawe**, kama wajua?

Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu muda mrefu kabla ya kuwa Mwana kutokea huko Bethlehemu. Hili limethibitishwa kwa uthabiti kupitia unabii wa Agano la Kale:

> Mika 5:2 Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; **ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale**, tangu milele.

Hata hivyo, swali la ni lini Yesu alizaliwa—kwenye enzi zote za umilele—linabakia kuwa ni fumbo lisiloweza kufahamika kwetu.

Sasa, unaweza kujiuliza hivi; Je, Yesu ana uzima wa milele nafsini

mwake? Tena, hii ni kweli. Lakini aliupokea uzima wake wa milele kutoka wapi?

> Yohana 5:26 Maana kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake, **vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake**.

Yesu aliupokea uzima wake kutoka kwa Baba. Na Baba ana maisha ya aina gani? Uzima wa milele. Maisha ya Uungu. Uhai ambayo Baba alimpa Mwanawe si uzima wa ubinadamu, bali wa Uungu wa milele! Hiyo ndiyo sababu Yeye ni muumbaji, na sababu Yeye ana uzima wa milele. Kwenye sura inayofuatia, tutazingatia namna ambavyo Kristo alivyoupokea huo uzima wa Uungu, wa milele.

## BABA HALISI WA UUNGU, MWANA HALISI WA UUNGU

> Waebrania 1:4 akiwa amefanyika bora kupita malaika, kwa kadri jina **aliloliirithi** lilivyo tukufu kuliko lao.

Ilikuwa ni kwenye urithi Kristo alipopokea uzima wa Uungu wa Baba yake! Kwa kweli, Yesu alipokea kwa kurithi jina bora zaidi kuliko malaika. Jina la Mungu. Hii ilikuwa ni haki yake ya mzaliwa wa kwanza kama "mwana pekee atokaye kwa Baba" (Yohana 1:14). Kumbuka maneno ya Kristo kwenye waraka wa Yohana:

> Yohana 5:26 Maana kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake, **vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake**.

Ili kuyafafanua zaidi maisha ambayo Kristo aliyarithi kutoka kwa Baba Yake, fikiria chati ifuatayo inayokazia uhusiano wa kibinadamu wa baba na mwana:

| **Baba wa Kibinadamu** | **Mtoto wa Kibinadamu** |
|---|---|
| Binadamu | Binadamu |
| Hufa | Hufa |
| Ana akili | Ana akili |
| Kuhoji | Kuhoji |
| Nia | Nia |
| Asili ya Kimwili | Asili ya Kimwili |
| Asili ya Kiroho | Asili ya Kiroho |

Kwenye tukio hili, je, mtoto ni binadamu mdogo kuliko baba yake? Hapana. Mwana alirithi asili ya baba yake tangu kuzaliwa kwake. Wanafanana kwa asili. Je, mtoto angekuwepo bila baba? Hapana, hakika sivyo ilivyo. Kwa maana mtoto aliyapokea maisha yake kutoka kwa baba yake!

Kwa kuizingatia hii kanuni, fikiria uhusiano uliopo kati ya Baba yetu

wa mbinguni na Mwanawe wa pekee kama inavyooneshwa na jedwali lifuatalo:

| **Mungu Baba** | **Mwana wa Mungu (Yesu Kristo)** |
|---|---|
| Uungu wa Mungu | Uungu wa Mungu |
| Hafi | Hafi |
| Wa milele | Wa milele |
| Mwenye Enzi Kuu | Mwenye Enzi Kuu |
| Mjuzi wa Kila Kitu | Mjuzi wa Kila Kitu |
| Yupo Kila Sehemu | Yupo Kila Sehemu |
| Asili ya Kimwili | Asili ya Kimwili |
| Asili ya Kiroho | Asili ya Kiroho |

Kwenye kisa hiki, je, Mwana ni wa Uungu kwa kiasi kidogo kuliko Baba? Hapana. Yesu alirithi asili ya Baba yake tangu alipozaliwa. Asili ya Uungu. Na kumbuka kuwa Mungu Baba pia ana asili ya kimwili. Danieli alimuona Mzee wa siku za kale akiwa ameketi juu ya kiti cha enzi "ambaye mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi" (Danieli 7:9). Isaya alimuona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na "pindo za vazi lake zikalijaza hekalu" (Isaya 6:1). Na Yohana pia aliona kiti cha enzi na akamuona "ameketi juu ya kile kiti" (Ufunuo 4:2).

Bila shaka, Mungu Baba ana asili ya kimwili. Yeye siyo kiini tu. Naye alikuwa na Mwana. Mfafanuzi wa Biblia, Ellet Joseph Wagoner anaandika hivi:

> Neno hilo lilikuwa ni 'hapo mwanzo.' Akili ya mwanadamu haiwezi kufahamu enzi ambazo zimesambazwa kwenye kifungu hiki cha maneno. Haijawekwa wazi kwa wanadamu kujua ni lini au namna gani Mwana alizaliwa; ila tunajua kuwa yeye alikuwa Neno la Mungu, si tu kabla hajaja duniani kufa, bali hata kabla ya ulimwengu kuumbwa. (EJ Waggoner, Christ and His Righteousness, 9)

Kwa hivyo Kristo alikuwepo kwa muda gani kabla ya kufanyika kuwa mwili? Ellen White anaelezea:

> Kristo anawaonyesha kuwa, ingawa wanaweza kuhesabu maisha yake kuwa chini ya miaka hamsini, lakini maisha yake ya Kimungu hayangeweza kuhesabiwa kwa hesabu ya kibinadamu. Kuwepo kwa Kristo kabla ya kupata mwili kwake hakupimwi kwa takwimu. (Signs of the Times, Mei 3, 1899)

Ingawa hatuwezi kupima urefu wa maisha ya Uungu wa Kristo kabla ya kufanyika mwili, tunapaswa kukubali tamko Lake kuwa alitoka kwa Mungu:

> Yohana 8:42 Yesu akawaambia, kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda mimi; kwa **maana nalitoka kwa Mungu**, nami nimekuja;...

Enyi marafiki, kutokana na mstari huu tu, tunaweza kuona kuwa Baba na Mwana si viumbe wa milele, kama ambavyo imani ya msingi #2 na imani nyingi kwenye dini ingetaka wewe uamini hivyo. Kinyume chake, Yesu anatuambia kuwa "alitoka kwa Mungu"!

Neno "kutoka" linamaanisha kuzaliwa, kutoka. Haina maana ya kutumwa tu. Yesu alizaliwa na Mungu. Kwenye enzi za umilele, Kristo alikuwa na mwanzo. Lakini je, hilo linamfanya Yesu kuwa Mungu mdogo? Hakika sivyo ilivyo. Yesu alirithi Uungu wa Mungu Baba!

Hakika, Yesu Kristo ni Mungu. Biblia imejaa vifungu vinavyoashiria hilo tu:

> Zaburi 50:3 **Mungu wetu atakuja** wala hatanyamaza...
>
> Yohana 20:28 Tomaso akajibu, akamwambia, **Bwana wangu na Mungu wangu**.

Ndiyo, Yesu ni Mungu. Hata hivyo, kuna ukweli wa kina zaidi. Maandiko pia yanafundisha kuwa Yesu Mwenyewe ana Mungu na Baba. Wana-

funzi wanasema kuwa:

> 1 Petro 1:3 Ahimidiwe **Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo**...
>
> Waefeso 1:3 **Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo**…
>
> 2 Wakorintho 11:31 **Mungu, Baba wa Bwana Yesu**,…

Mwanawe asema hivi:

> Yohana 20:17 ...Ninapaa kwenda **kwa Baba yangu** naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu.
>
> Ufunuo 3:12 Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la **Mungu wangu**,... nami nitaandika juu yake jina **la Mungu wangu**, na jina la mji wa **Mungu wangu**, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa **Mungu wangu**…
>
> Isaya 49:4 ...hakika hukumu yangu ina BWANA, na thawabu yangu ina **Mungu wangu**.
>
> Isaya 49:5 ...maana mimi nimepata heshima mbele ya macho ya BWANA, na **Mungu wangu** amekuwa nguvu zangu.

Na kwenye hii mistari miwili inayofuatia, hata Baba anamuita Yesu kuwa ni Mungu:

> Waebrania 1:8 Lakini kwa habari za Mwana asema, Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; Na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili.
>
> Waebrania 1:10 Na tena, Wewe, Bwana, hapo mwanzo aliitia misingi ya nchi, na mbingu ni kazi za mikono yako;

Hata hivyo, ona kile ambacho Baba anakisema kwenye mstari wa 9:

> Waebrania 1:9 Umependa haki, umechukia maasi; kwa hiyo Mungu, **Mungu wako**, amekutia mafuta, Mafuta ya shangwe kupita wenzio.

Inaeleweka kikamilifu kwa namna gani! Wanafunzi, Yesu, na Baba Mwenyewe wote wanashuhudia kuwa Yesu ana Mungu na Baba.

Ewe rafiki, kama Mungu angekuwa ni mwenye utatu, vifungu vya kweli ambavyo tumevisoma hivi punde vingekuwa ni kufuru, kwa kuwa utatu unafundisha umoja wa viumbe watatu wa milele na ambao ni sawa. Hata hivyo, hii mistari yote iliyohamasishwa inafundisha kuwa ingawa Yesu anafaa kuitwa Mungu, Yeye Mwenyewe anaye Mungu na Baba.

Yule yule Paulo ambaye anasema kuwa "Yesu Kristo ni Bwana" (Wafilipi 2:11) pia anashuhudia kuwa "lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba" (1 Wakorintho 8:6). Je, utamshtaki mtume Paulo kwa kuamini kwenye miungu miwili? Pia, Paulo alisema hivi kuhusu Yesu:

> Wakolosai 1:15 naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, **mzaliwa wa kwanza** wa viumbe vyote:

Ni agano lenye nguvu kama nini! Kristo anaitwa kuwa ni "mfano wa Mungu asiyeonekana", na pia anaitwa "mzaliwa wa kwanza" wa kila kiumbe. Sasa angalia kile ambacho Lexicon ya Kiyunani inasema kuhusu huu mstari:

> Kristo anaitwa mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote, **ambaye alifanyika kwa njia ya Mungu kabla** ya ulimwengu wote wa viumbe...

Wakolosai 1:15 inatufundisha kuwa wakati Kristo ni sawa pamoja na Mungu (kwa maana yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana), alifanyika kwa njia ya Mungu (kama mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote). Ndiyo maana Paulo anasema kuwa "lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba". Ni kwa sababu Baba ndiye mwanzilishi wa maisha yote! Kwa hivyo, unaweza kuwa unajiuliza ni kwa nini Kristo anaitwa "Bwa-

na"? Ni kwa sababu Kristo alizaliwa kweli na Baba, na hivyo akarithi asili yake halisi ya Uungu.

Zaidi ya hayo, kwenye Waebrania 1:6, mtume Paulo anamuita Yesu kuwa ni “mzaliwa wa kwanza” **aliyeletwa ulimwenguni**, kama vile Yohana asemavyo kwenye 1 Yohana 4:9. Lakini jambo la kushangaza ni kuwa baadhi ya ndugu bado wanadai kuwa Kristo alikuwa ni Mtoto kutoka Bethlehemu tu.

Zaidi ya hayo, ndugu hao hao wanaofundisha kuwa kiumbe mwenza wa milele aliyechukua nafasi ya Mwana huko Bethlehemu wanadai kuwa jukumu hili ilikuwa ni kwa ajili ya mpango wa wokovu.

Ila angalia kile ambacho 1 Wakorintho 15:28 inasema juu ya Mwana wa Mungu mara tu mpango wa wokovu utakapokamilika:

> 1 Wakorintho 15:28 Basi, vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake, ndipo Mwana mwenyewe naye atatiishwa chini yake yeye aliyemtiishia vitu vyote chini yake, ili kwamba Mungu awe yote katika wote.

Tangu siku za kabla ya uumbaji, hadi Yerusalemu ya kimbingu ya wakati unaokuja, siku zote Kristo atakuwa ni Mwana mzaliwa-pekee wa Mungu. Na kwa upendo, kwa hiari, atajiweka chini ya mapenzi ya Baba yake.

Kama tulivyoona hapo awali, Yesu anaitwa Mungu kwa halali. Hata hivyo, Biblia pia inafundisha kuwa Yesu Mwenyewe ana Mungu na Baba. Kwa hivyo, Mungu siyo kiini cha ajabu isichogawanyika cha watu watatu wa milele. Badala yake, Mungu Baba alikuwa na Mwana, na kwenye asili, Mwana aliurithi Uungu wa Baba yake.

Tafadhali elewa jambo hili. Uungu wa Mungu ni Roho wa Mungu. Kuna Uungu mmoja tu, na kwa hiyo ni Roho mmoja tu. Mungu Baba ndiye chanzo cha asili cha Uungu huu, kama vile vyeo vyake vinavyoonesha wazi wazi jambo hili:

- Mzee wa siku za kale (Danieli 7:9)
- Mungu wa pekee wa kweli (Yohana 17:3)
- Mungu Aliye Juu (Zaburi 78:56)
- Mwenye enzi kuu ya ulimwengu (PP 34)
- Mwana wa Mungu Aliye Juu (Marko 5:7)

Kwenye Marko 5:7, ni mapepo wanaozungumza. Shetani anajua Mungu Aliye Juu Zaidi ni nani. Na hata mashetani wanakiri kuwa ni kweli Kristo ni "Mwana wa Mungu Aliye Juu"! Kwa hakika, mashetani wanaamini na kukiri ukweli huu, huku wanaoamini utatu wakifundisha hivi:

> Kuna Mungu mmoja: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, umoja wa nafsi tatu za milele...

Jedwali lifuatalo linaonesha fundisho la utatu, kwa kuzingatia kauli iliyotolewa hapo awali.

| **Mungu Baba** | **mungu Mwana** | **mungu Roho Mtakatifu** |
|---|---|---|
| Wa Uungu | Wa Uungu | Wa Uungu |
| Wa Milele<br>(hana mwanzo) | Wa Milele<br>(hana mwanzo) | Wa Milele<br>(hana mwanzo) |
| Mwenye enzi kuu na kadhalika | Mwenye enzi kuu na kadhalika | Mwenye enzi kuu na kadhalika |

Kulingana na wale wanaoamini kwenye utatu, 'mungu Mwana'—neno lisilokuwepo hata mara moja kwenye Biblia Takatifu au Roho ya Unabii—ndiye chanzo cha uungu wake mwenyewe. Yeye ni wa milele pamoja na watu wengine wawili. Kwa hiyo, hana mwanzo, na uana wake ni sitiari tu; kuhusika kwenye majukumu.

Wakati mtu anapoamini kwenye utatu na matamshi lake 'mungu mwana', lazima akubali kuwa wanaamini kwenye miungu miwili. Ni kwa nini? Ni kwa sababu wanaoamini utatu wanakana kuwa 'mungu mwana' alikuwa na mwanzo. Wanafundisha kuwa yeye ni wa kimungu na amekuwepo siku zote. Kwa hiyo, kwa kutokuwa na uhusiano na Baba,

anabeba uungu wake ambao ni tofauti. Hii inawafanya miungu wawili, au miungu miwili! Pingamizi hili haliwezi kujibiwa.

Ili kufanya mambo kuwa mabaya zaidi, wale wanaoamini kwenye utatu basi wanaamini kwenye mungu Roho; mtu wa tatu wa uungu ambaye ni wa milele. Hii inatuacha na viumbe watatu wa mungu mmoja mmoja. Hii ni dini ya washirikina. Hakika hii ni injili nyingine.

## ROHO WAO, ROHO MTAKATIFU

Mpaka sasa, tumeona kuwa Baba ndiye “Mungu wa pekee na wa kweli” na kuwa Yesu Kristo ndiye “Mwana pekee wa Baba”. Sasa hebu tuone namna Biblia inavyomuelezea Roho Mtakatifu:

> Warumi 8:9 Lakini ikiwa **Roho wa Mungu** anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata Roho, Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.
>
> Wagalatia 4:6 ...**Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe** mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba.
>
> Marko 13:11 Na watakapowachukua ninyi, na kuwasaliti, msitafakari kwanza mtakayosema, lakini lolote mtakalopewa saa ile, lisemeni; **kwa maana si ninyi msemao, bali ni Roho Mtakatifu.**

“Roho Mtakatifu” ni nani? Tazama kifungu hicho hicho kwenye injili ya Mathayo:

> Mathayo 10:19 Lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri-fikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakayosema.
> 10:20 Kwa kuwa si ninyi msemao, **bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu.**
>
> 2 Petro 1:21 Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; **bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.**

Na ni nani aliyewaongoza manabii?

> 1 Petro 1:10 Katika habari ya wokovu huo manabii walitafuta-tafuta na kuchunguza-chunguza,...
> 1:11 Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani uliooonywa na **Roho wa Kristo** aliyekuwa ndani yao, ambaye alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo.

> Wafilipi 1:19 Maana najua ya kuwa haya yatanigeukia kuwa wokovu wangu, kwa sababu ya kuomba kwetu, **na kuruzukiwa Roho wa Yesu Kristo**;

> Yohana 20:22 Naye akiisha kusema hayo, **akawavuvia**, akawaambia, **Pokeeni Roho Mtakatifu**.

Kwa muhtasari, tunaweza kuhitimisha haya yafuatayo:

1. Roho wa Mungu ni Roho wa Kristo (Warumi 8:9).
2. Mungu humtuma "Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu". Si mtu mwingine (Wagalatia 4:6).
3. Roho Mtakatifu ni Roho wa Baba (Marko 13:11, Mathayo 10:19,20).
4. Roho Mtakatifu aliyejidhihirisha kwa manabii ni Roho wa Kris to (2 Petro 1:21, 1 Petro 1:10-11).
5. Roho Mtakatifu huja moja kwa moja kutoka kwa Kristo; ni pumzi, tabia, na uzima Wake (Yohana 20:22).

Zaidi ya hayo, kwenye Yohana 20:22, tumepewa ufahamu usiyo na shaka wa mahali ambapo Roho Mtakatifu anatokea. Je, ni kwa namna gani tena mtu anaweza kuelewa aya hii inayofuatia?

> Yohana 20:22 Naye akiisha kusema hayo, **akawavuvia**, akawaambia, **Pokeeni Roho Mtakatifu**.

Roho Mtakatifu alitokea wapi? Yohana anasema hivi: "Kristo aliwavuvia". Ni kuvuviwa pumzi ya Kristo mwenyewe. Roho Mtakatifu alitoka ndani Yake!

Roho Mtakatifu si mtu wa pamoja wa tatu ambaye ni wa milele. Kristo aliwaambia wanafunzi wake akasema hivi: "Pokeeni Roho Mtakatifu". Ni kielelezo kizuri zaidi kwa sababu ni cha kitendo. Na huyu ndiye Roho yule yule tunayempata kwenye hadithi ya uumbaji:

> Mwanzo 1:2 Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu; na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; **Roho ya Mungu** ikatulia juu ya uso

wa maji.

Baadhi ya watu hutafsiri hili kwa kumaanisha kuwa Roho Mtakatifu—kiumbe wa tatu wa Uungu—alikuwa akitembea juu ya maji. Lakini mstari huo unasema kuwa ilikuwa ni "Roho ya Mungu" iliyotembea juu ya maji. Je, Daudi anaielezeaje Roho kwenye uumbaji?

> Zaburi 33:6 Kwa neno la BWANA mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake…

Angalia neno la: "pumzi". Hili ni neno lile lile la Kiebrania ambalo limetafsiriwa kama "roho" kwenye Mwanzo 1:2!

> roho
> kutoka kwenye 'ruwach' (7306); upepo; pumzi, kwa kufanana na roho, lakini tu ya kiumbe mwenye akili (pamoja na usemi na utendaji wake):—hewa, pumzi, akili, upepo wa roho.

Neno halisi linamaanisha "pumzi". Kwa hivyo, ni nini kilichotembea juu ya uso wa maji? "Pumzi ya kinywa chake". Ilikuwa ni pumzi ya Kristo—neno lake lililonenwa—lililotembea juu ya maji:

> Zaburi 33:9 Maana Yeye **alisema**, ikawa; na Yeye ali **iliamuru**, ikasimama.

Kwa hivyo, Roho wa Mungu ni neno lililonenwa ambalo ni la Mungu. Siyo kiumbe mwingine. Kwa kweli, Roho Mtakatifu anafafanuliwa kuwa ni uwepo binafsi wa Mungu na Kristo. Fikiria hivi vifungu vifuatavyo:

> Zaburi 139:7 Niende wapi nijiepushe na **roho yako**? Niende wapi **niukimbie uso wako**?
> 139:8 Kama ningepanda mbinguni, wewe uko; Ningefanya kuzimu kitanda changu., Wewe uko.
> 139:9 Ningezitwaa mbawa za asubuhi, na kukaa pande za mwisho za bahari;
> 139:10 **Huko nako mkono wako utaniongoza, Na mkono wako wa kuume utanishika.**

> Zaburi 51:11 Usinitenge **na uso wako**, wala **roho yako mtakatifu** usiniondolee.

> 2 Mambo ya Nyakati 16:9 Kwa maana **macho ya BWANA** hukimbia-kimbia duniani mwote, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao waliokamilika moyo kuelekea kwake…

> Zaburi 11:4 BWANA yu katika hekalu lake takatifu. BWANA ambaye kiti chake kiko mbinguni, macho yake yanaangalia; Kope zake zinawajaribu wanadamu.

Roho Mtakatifu ni Roho wa Mungu. Ni uwepo wake na neno lake. Siyo mtu mwingine. Kwenye kauli sambamba ambazo zinafuatana tunagundua kuwa Roho wa Mungu pia ni akili ya Mungu:

> Isaya 40:13 Ni nani aliyemwongoza **Roho ya BWANA**, na kumfundisha kwa kuwa mshauri wake?

> Warumi 11:34 Maana ni nani aliyeijua **nia ya Bwana**? Au ni nani aliyekuwa mshauri wake?

Kwa hiyo, Roho Mtakatifu ni neno la Mungu, uwepo wake, na akili yake. Na ni Roho wa Mungu na Kristo aliye nena kwa wanafunzi, kama ambavyo mistari ifuatayo inavyoonesha:

> Marko 13:11 Na watakapowachukua ninyi, na kuwasaliti, msitafakari kwanza mtakayosema, lakini lolote mtakalopewa saa ile, lisemeni; kwa maana si ninyi msemao, **bali ni Roho Mtakatifu**.

> Mathayo 10:19-20 Lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri-fikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakayosema. Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni **Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu.**

> 2 Petro 1:21 Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu,

**wakiongozwa na Roho Mtakatifu.**

> 1 Petro 1:11 wakichunguza ni wakati gani na wa namna gani **Roho wa Kristo** aliyekuwa ndani yao alionyesha, alipoyashuhudia mateso ya Kristo, na utukufu utakaofuata.

Enyi marafiki, Roho Mtakatifu ni Roho wa Mungu na Kristo, kama vile Paulo anavyonena kwenye Warumi 8:9:

> Warumi 8:9 Lakini ikiwa **Roho wa Mungu** anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata Roho, Lakini mtu awaye yote asipokuwa na **Roho wa Kristo**, huyo si wake.

Hatimaye, Roho Mtakatifu ni pumzi, uwepo, akili, mkono wa kuume wa nguvu (Uungu), na macho ya Bwana. Ni sababu hii iliyofanya Roho anaitwa:

- Roho ya Kristo (Petro 1:11)
- Roho ya Mwanawe (Wagalatia 4:6)
- Roho ya Baba yenu (Mathayo 10:20)
- Roho ya Yesu Kristo (Wafilipi 1:19)
- Roho ya Mungu (Mathayo 3:16)

Kwa hakika, neno “ya” lina umiliki. Roho ni ya Mungu. Siyo mtu mwingine. Angalia kifungu kifuatacho kutoka kwenye kitabu cha Danieli:

> Danieli 2:1 Hata katika mwaka wa pili wa kumiliki kwake Nebukadreza, Nebukadreza, aliota ndoto; **roho yake ikafadhaika**, usingizi wake ukamwacha.

Mtu asingeweza kusoma maneno “roho yake ilifadhaika”, na kufikiri kuwa mtu mwingine alikuwa na wasiwasi. Ni mawazo ya Nebukadneza ndiyo yaliyokuwa na wasiwasi! Hatuna ugumu wa kulikubali jambo hili. Kwa hivyo, sasa ni kwa nini tunaposoma kifungu cha maneno ya: "Roho ya Mungu", tunahisi haja ya kumtenga Roho na kumgeuza kuwa nafsi ya tatu? Hivi ndivyo hasa utatu unavyofanya, kama Mchungaji

Max Hatton anavyosema waziwazi:

> Roho Mtakatifu ni Nafsi ya Utatu; Yeye si Baba, wala si Mwana. Yeye ni Mmoja wa wale watatu wa milele.
>
> Roho Mtakatifu anabeba nafasi ya Yesu…Yeye ndiye Mshauri wa Yohana 14:16.

Utatu unafundisha kuwa Roho Mtakatifu ni mtu mwingine. Sasa, na tuchunguze kwenye Yohana 14:16-17; kifungu ambacho Mchungaji Hatton anakirejelea kwenye nukuu iliyotangulia.

> Yohana 14:16 Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;
> 14:17 ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi **mnamtambua, maana anakaa kwenu**, naye atakuwa ndani yenu.

Akizungumza juu ya Msaidizi ambaye angekuja siku ya Pentekoste, Yesu anawaambia wanafunzi Wake: "Ninyi mnamtambua". Walimjuaje? “Maana anakaa kwenu”.

Mfariji hakuwa ni mgeni. Wakati huo huo alikuwa anakaa pamoja na wanafunzi. Alikuwa akiishi nao, akila pamoja nao, na kusafiri pamoja nao. Alikuwa nao kwenye wakati uliopo. Ndiyo maana Yesu anawaambia wanafunzi wake kuwa “mnamtambua”. Kwenye mstari unaofuatia, Yesu anabainisha wazi wazi nani ambaye ni Msaidizi:

> Yohana 14:18 Sitawaacha ninyi yatima; **naja kwenu**.

Yesu anasema hivi: “Naja kwenu”. Ni "mimi", ambaye tayari ninaishi nanyi. "Mimi", ambaye tayari unamtambua. Je, hii inaonekana kana kwamba mtu mwingine anaichukua nafasi Yake? Yesu anaendelea kusema:

> Yohana 14:20 Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, **nanyi ndani yangu,** nami ndani yenu.

> 14:21 ...**nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.**

Wanafunzi walielewa yule Msaidizi alikuwa ni nani. Wanafunzi walimuamini pale alipoahidi kuwa: "Naja kwenu". Walitaka tu kujua kuwa angerudi kwa namna gani. Angalia mazungumzo yanayofanyika kati ya Yesu na wanafunzi wake:

> Yohana 14:22 Yuda (siye Iskariote), akamwambia, Bwana, imekuwaje ya kwamba wataka **kujidhihirisha kwetu**, wala si kwa ulimwengu?
> 14:23 Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi **tutakuja kwake na kufanya makao kwake.**

Kristo alikuwa akiwaacha wanafunzi kimwili, lakini alikuwa anakuja kukaa nao kiroho. Ndiyo maana ulimwengu usingemtambua, lakini wale waliomjua yeye binafsi wangemtambua. Upendo ule ule, furaha, na amani ambayo wanafunzi walikuwa wameipitia pamoja na Yesu wakiwa ana kwa ana, ilikuwa inatakiwa kukaa nao kwa njia ya Roho Wake. Ahadi ya Kristo ilikuwa ni hii:

> Yohana 14:23 Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda, **nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake.**

Ila kinyume chake, utatu unasisitiza hivi:

> Roho Mtakatifu ni Nafsi ya Utatu; Yeye si Baba, wala si Mwana Wake.

Ila Biblia inasemaje?

- ...Naja kwenu. (Yohana 14:18)
- ...Nami ndani yenu. (Yohana 14:20)
- ...nitajidhihirisha kwake. (Yohana 14:21)
- ...nami nipo papo hapo katikati yao. (Mathayo 18:20)
- ...Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa. (Waebrania 13:5)
- ...akawaambia, Pokeeni Roho Mtakatifu. (Yohana 20:22)

- ...Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu,... (Wagalatia 4:6)

Enyi marafiki, shikamana sana na ahadi za Yesu Kristo. Kumbuka maneno ya mwisho aliyoyasema kwa ajili ya kanisa lake. Ahadi yake ya kutuaga ilikuwa ni hii:

> Mathayo 28:20 ...**tazama, mimi nipo pamoja nanyi** siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amina.

Kristo alipokuwa akipaa kuelekea mbinguni, alitaka kuwahakikishia wafuasi wake kuwa angebakia pamoja nao. Hakuwa akimtuma mtu mwingine kuchukua mahali Pake. Anasema hivi: "tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari".

Enyi marafiki, huyu ndiye Mfariji aliye pamoja nasi sasa hivi. Si kiumbe fulani cha ajabu ambacho hatukijui, ambaye hajawahi kushiriki kwenye ubinadamu wetu, na kamwe hawezi kuelewa majaribu ambayo tunakabiliana nayo kila siku. Hapana. Msaidizi ni mtu ambaye alitembea kwenye Dunia hii kwa miaka thelathini na mitatu na nusu, ambaye alikutana na kila aina ya majaribu "isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu" (1 Wakorintho 10:13), na ambaye alijifunza "kutii kwa mateso hayo yaliyompata. " (Waebrania 5:8). Ni yeye ambaye amekuwa ndiye "mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu" (Waebrania 12:2). Yeye ndiye anayeahidi hivi:

> Yohana 14:18 Sitawaacha ninyi yatima, **naja kwenu**.
>
> Waebrania 13:5 ...**Sitakupungukia kabisa**, wala sitakuacha kabisa.
>
> Mathayo 18:20 Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, **nami nipo papo hapo** katikati yao.

Kwenye hili somo lote, tumejifunza kuwa kuna Mungu mmoja tu ambaye ni wa kweli; Baba. Tumejifunza pia kuwa Yesu ni Mwanawe wa pekee; aliyezaliwa kwenye mfano ulio dhahiri wa utu wa Baba, na kwenye

mwangaza na utukufu Wake wote. Hatimaye, tumeona kwamba Roho Mtakatifu ni Roho wa Mungu na Kristo. Hii ndiyo injili ya kweli. Injili inayotolewa “kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe” (Waefeso 4:12). Na ni injili hii ambayo itatuleta kwenye “umoja wa imani, na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu” (Waefeso 4:13).

Hiki ndicho ambacho Paulo anachokiita “unyofu na usafi wa Kristo” (2 Wakorintho 11:3). Ni fursa yetu ya kuungama pamoja na Petro na mitume: “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai”. Mathayo 16:16.

## MAJIBU YA VIPINGAMIZI

## 1 YOHANA 5:8

> 1 Yohana 5:8 Kwa maana wako watatu washuhudiao [mbinguni, Baba, na Neno, na Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni umoja….

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* 1 Yohana 5:8 inasema kuwa Baba, Neno, na Roho Mtakatifu ni umoja. Hii inaonesha utatu wa nafsi tatu za milele.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* 1 Yohana 5:8 haisemi kuwa hawa watatu ni wenye utatu, au kuwa wao ni mungu mmoja. Inasema tu kuwa wao ni mmoja. Tunaonywa tusiongeze neno katika maneno ya Mungu (Mithali 30:6).

1 Yohana 5:8 huanza na maneno haya: "Kwa maana wako watatu washuhudiao [mbinguni". Baba, Neno, na Roho Mtakatifu ni wamoja kwenye ushuhuda wanaoutoa. Angalia mstari unaofuatia:

> 1 Yohana 5:9 Kisha wako watatu washuhudiao [duniani, Roho, na maji, na damu; na watatu hawa hupatana kwa habari moja.

Yohana anaposema hivi: "watatu hawa hupatana kwa habari moja", anarejelea kwenye ushuhuda ambao Baba, Mwana na Roho Mtakatifu "hushuhudia" ndani yake. Yohana anasema kuwa "watatu hawa hupatana kwa habari moja"; ikimaanisha kuwa wameunganishwa kwenye ushuhuda wanaoutoa. Na ushuhuda huo ni upi?

> 1 Yohana 5:5 Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?

Kuitafsiri 1 Yohana 5:7 kumaanisha utatu wa watu watatu wa milele ni kukana kuwa kweli Yesu ni Mwana wa Mungu. Kwa maana utatu unafundisha kuwa Yesu ni mwana ambaye ni mfano tu. Bado ni aya mbili tu zilizotangulia, tunaonywa kuwa njia pekee ya kushinda ulimwengu ni kuamini kuwa "Yesu ni Mwana wa Mungu"! Na kwenye mstari wa 6

tunasoma hivi:

> 1 Yohana 5:6-7 Huyu ndiye aliyekuja kwa maji na damu, Yesu Kristo; si katika maji tu, bali katika maji na katika damu. Naye Roho ndiye ashuhudiaye, kwa sababu Roho ndiye kweli.

Utagundua kuwa pia Roho anashuhudia kuwa Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu. Sasa kwenye mstari wa 9, tunasoma kuhusu ushuhuda wa Baba juu ya Mwanawe:

> 1 Yohana 5:9 Tukiupokea ushuhuda wa wanadamu, ushuhuda wa Mungu ni mkuu zaidi; kwa maana **ushuhuda wa Mungu ndiyo huu, kwamba amemshuhudia mwanawe.**

Je, inakuwaje ikiwa hatuamini rekodi ambayo Mungu aliitoa kuhusu Mwanawe? Yohana anaendelea kusema hivi:

> 1 Yohana 5:10 Yeye amwaminiye Mwana wa Mungu anao huo ushuhuda ndani yake. **Asiyemwamini Mungu amemfanya kuwa mwongo, kwa kuwa hakuuamini huo ushuhuda ambao Mungu alimshuhudia Mwanawe.**

Ni muhimu kiasi gani kumuamini Mwana wa Mungu? Yohana anathibitisha tena akisema:

> 1 Yohana 5:11 Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe.
> 5:12 Yeye aliye naye Mwana anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.

Tusisahau ushuhuda wa Yesu mwenyewe, kama ulivyoandikwa na mwandishi huyo huyo:

> Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii **Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee**, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Inafurahisha kuona kuwa kwenye 1 Yohana 5:7, neno ambalo Yohana analitumia kwa Mwana ni "Neno". Hili ni muhimu kwa sababu kwenye Injili ya Yohana, anatuambia huyo Neno ni nani hasa:

> Yohana 1:14 Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa **Mwana pekee atokaye kwa Baba**; amejaa neema na kweli.

Hivyo, mtu angeweza kutafsiri 1 Yohana 5:8 kwa usahihi kuwa: 1 Yohana 5:8 Kwa maana wako watatu washuhudiao [mbinguni, Baba, na Neno na Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni mmoja.

Tumeona kuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni wamoja kwenye kumbukumbu wanazozitoa, na rekodi hiyo ni: "Yesu ni Mwana wa Mungu" (1 Yohana 5:5). Inashangaza! Andiko lile lile ambalo wanaoamini kwenye utatu wanalitumia kufundisha utatu wa nafsi tatu za milele ambazo ni za pamoja (na hivyo kukana kuwa Yesu ni Mwana halisi wa Mungu) inashuhudia kumbukumbu kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu! Zaidi ya hayo, sura hiyo inaelezea wazi kuwa, uzima wetu wa milele inategemea sisi kuamini ukweli huu.

> "1 Yohana 5:13 Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini jina la Mwana wa Mungu".

## MATHAYO 28:19

> Mathayo 28:19 Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Orodha hii ya majina matatu (Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu) inaonyesha utatu wa nafsi tatu za milele.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Kristo anaorodhesha majina matatu (Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu) lakini kamwe haimaanishi kuwa wao ni wa utatu wa nafsi tatu za milele. Badala yake, daima, Yeye husema kuwa Roho Mtakatifu (Roho) ni Roho wa Mungu Mwenyewe.

Kwa kweli, Mathayo 28:19 huurejesha ukweli kuhusu uhusiano wa Baba na Mwana. Kuhusu Roho Mtakatifu, tayari tumejifunza kuwa ni Roho binafsi ya Baba na Mwana. Fikiria mambo haya yafuatayo kama muhtasari wa kile ambacho tumejifunza mpaka sasa:

Roho hutokea kwa Baba. (Yohana 15:26)
Roho ni uso na nguvu za Mungu. (Zaburi 139:7, Zaburi 51:11)
Roho ni pumzi ya kinywa cha Mungu na neno la Mungu. (Mwanzo 1:2, Zaburi 33:6,9)
Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu. (Wagalatia 4:6)
Roho ni Roho ya Baba na Mwana. (Warumi 8:9)
Yesu asema ya kuwa "tutakuja kwake, na kufanya makao kwake". (Yohana 14:23)
Yesu ndiye Mfariji wetu. (Yohana 14:18)
Roho wa Kristo alijidhihirisha kwa manabii. (1 Petro 1:11)
Roho hutokea kwa Kristo. (Yohana 20:22)

Wanaoamini kwenye utatu huitumia Mathayo 28:19 ili kuufundisha utatu wa nafsi tatu za milele ambazo zipo pamoja. Hata hivyo kwenye kumkana Baba na Mwana halisi, wanaharibu kiini hasa cha kifungu wanachokinukuu! Kumbuka maneno haya yaliyosemwa na wanatheolojia wa Kiadventista:

> Mpango wa wokovu ulijumuishwa kwenye agano lililofanywa na Nafsi Tatu za Uungu, ambazo zilikuwa na sifa za Uungu kwa usawa. Ili kuondoa dhambi na uasi kutoka kwenye ulimwengu na kuurejesha upatanisho na amani, mmoja wa Viumbe wa Kimungu alikubali, **na aliingia kwenye nafasi ya Baba, mwingine akawa na jukumu la Mwana**…
>
> Uhusiano wa Baba na Mwana kwenye Uungu unapaswa kueleweka kwa **maana ya sitiari, si kwa maana halisi.**
>
> Yesu alifanyika Mwana wa Mungu wakati wa kuzaliwa kwake mwanadamu...

Maneno haya yanapingana kabisa na kile ambacho Mathayo 28:19 inatufundisha. Yesu asema hivi:

> Mathayo 28:19 Basi, **enendeni, mkawafanye mataifa** yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;

Hapa, Kristo anawaagiza wafuasi wake kwa kusema "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi". Anawaagiza kuwabatiza wengine na kuwapa kweli ya Baba, Mwanawe, na Roho Mtakatifu wao. Angalia kifungu ambacho ni sambamba na hiki kwenye injili ya Marko:

> Marko 16:15 Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

Sasa, upi ni ukweli wa kanuni wa injili ambao unapaswa kuhubiriwa kwa kila kiumbe? Kwa mujibu wa Yesu, ni ule ukweli kwenye Yohana 3:16:

> Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Na kuhusu hii injili, Marko anaandika hivi: "Aaminiye na kubatizwa

ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa" (Marko 16:16). Enyi marafiki, hivi ndivyo Kristo anavyowaagiza wanafunzi wake kufundisha kwenye Mathayo 28:19. Ni kwenye injili hii ambapo tunajua kuwa tunapaswa kuitumia kubatiza, na kubatizwa. Mathayo 28:19 inatusihi kumuamini Baba ambaye alikuwa na Mwana pekee na alimtuma kutoka mbinguni kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Fikiria ushuhuda huu wa Mkristo aliyebadilishwa:

> 1 Yohana 4:13 Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu, **kwa kuwa ametushirikisha Roho wake.**
> 4:14 Na sisi tumeona na kushuhudia ya kuwa **Baba amemtuma Mwana kuwa Mwokozi wa ulimwengu.**
> 4:15 Kila **akiriye ya kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu**, Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya Mungu.

Enyi marafiki, tazama namna ilivyokuwa ni muhimu kuamini Injili ya kweli:

> 1 Yohana 5:5 Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, **isipokuwa ni yeye aaminiye** ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?

Baada ya Yesu kusema kwenye Yohana 3:16, aliongezea kwa kutoa onyo hili:

> Yohana 3:18 Amwaminiye yeye hahukumiwi; **asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.**

Inashangaza! Andiko lile ambalo wanao amini kwenye utatu wanalitumia kufundishia utatu (wa utatu wa milele ambao ni wa pamoja) linawashutumu kwa sababu hawaamini "jina la Mwana pekee wa Mungu".

## YOHANA 16:13

> Yohana 16:13 Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Roho anajulikana kama "yeye". Kwa hiyo, ni lazima iwe ni kielelezo cha mtu mwingine.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Mara nyingi Yesu mara anazungumza juu Yake mwenyewe kwenye nafsi ya tatu. Kwa hiyo, matumizi ya neno "yeye" hailazimu awe ni mtu tofauti.

Ufikirie mstari ufuatao kama mfano:

> Luka 18:8 Nawaambia ya kwamba **atawapatia** haki upesi; walakini, atakapokuja Mwana wa Adamu, je! **Ataiona** imani duniani?

Kwenye Luka 18:8, Kristo anazungumza juu Yake mwenyewe kwenye nafsi ya tatu. Kwa jambo hili pekee, hauwezi kudhani kuwa ni lazima matumizi ya neno "yeye" kwenye Biblia yaelekezwe kwa mtu mwingine. Mfano kama huo umetolewa kwenye Injili ya Yohana:

> Yohana 9:35 Yesu…alisema, Wewe wamwamini Mwana wa Mungu?
> 9:36 Naye akajibu akasema, Ni nani, Bwana, nipate kumwamini?
> 9:37 Yesu akamwambia, Umemwona, naye anayesema nawe ndiye.

Kwa hapa tena, Kristo anajiita "naye" na "ndiye". Na akizungumza juu ya Roho, Yesu anasema hivi: "maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe". Sasa angalia ulinganifu kati ya kauli hii na kile kingine ambacho Yesu anasema kumhusu Yeye Mwenyewe kwenye injili ya Yohana:

| Nafsi ya Tatu: Yohana 16:13 | Nafsi ya Kwanza: Vifungu Vingine |
|---|---|
| “…maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena…” | “Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. Nami najua ya kuwa agizo lake ni uzima wa milele; basi hayo ninenayo mimi, kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo.” Yohana 12:49, 50 |
| | "…maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake. Yohana 14:10 |
| | "…nalo neno mnalolisikia silo langu, ila ni lake Baba aliyenipeleka." Yohana 14:24 |
| | "…ila kama Baba alivyonifundisha ndivyo ninenavyo." Yohana 8:28 |

Wakati wa huduma Yake, Yesu alizungumza maneno ambayo Baba Yake alimpatia. Ndiyo maana kwenye Yohana 16:13, Anasema hivi: Roho “hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena”. Tangu anguko, mawasiliano yote kati ya Mungu na mwanadamu yamekuwa ni kwa njia ya Kristo. Hata kwa sasa mbinguni, Kristo anazungumza maneno ya Baba yake. Kutimia kwa sehemu ya Yohana 16:13 kunaonekana kwenye Ufunuo 1:1:

| Yohana 16:13 | Ufunuo 1:1 |
|---|---|
| “Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.” | “Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwangu hayana budi kuwako upesi;..." |

Bila shaka, Roho wa kweli wa kwenye Yohana 16:3 ni Roho wa Kristo. Kwenye Ufunuo sura ya 2, Yohana anafundisha waziwazi kuwa Kristo ndiye Roho ambaye anazungumza na makanisa:

> Ufunuo 2:8 Na kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna andika; **Haya ndiyo anenayo yeye aliye wa kwanza na wa mwisho, aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai.**

“Wa kwanza na wa mwisho” ni nani? Ni nani “aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai”? Si mwingine ila ni Kristo! Kwa hiyo, ni Kristo ambaye analiandikia kanisa la Smirna. Na je, Kristo anazungumzaje? Yohana anatuonya hivi:

> Ufunuo 2:11 Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo **Roho ayaambia makanisa**...

Ni kwa njia ya Roho wake Kristo anayezungumza na makanisa. Kwenye nuru hii, Roho wa kweli ni Yeye “aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai” (Ufunuo 2:8), ambaye hasemi maneno Yake mwenyewe, bali maneno ya Baba Yake.

## YOHANA 1:1

> Yohana 1:1 Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Neno alikuwa ni Mungu. Kwa hiyo, Yesu ni wa uungu wa milele.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Neno ndiye "mwana pekee atokaye kwa Baba" (Yohana 1:14). Hii ndiyo sababu Kristo ni sawa na Mungu, na kwa haki anaweza kuitwa Mungu. Lakini Yesu mwenyewe anashuhudia kuwa Baba ndiye "Mungu wa pekee wa kweli" (Yohana 17:3).

"Mwanzo" unamrejelea nani? Maneno matatu yanayofuata yanaonyesha kuwa "hapo mwanzo **kulikuwako Neno**". Wanao amini kwenye utatu wana njia mbili kwenye kutafuta kuukwepa ukweli wa kuwa neno "hapo mwanzo" linarejelea "Neno".

Kwa upande mmoja, wanadai kuwa "hapo mwanzo" inarejelea kwenye uumbaji. Hili ni tatizo kwani uumbaji haujatajwa hadi kwenye mstari wa 3. Yohana 1:1 inasema kwa urahisi kabisa:

> Yohana 1:1 Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.
> 1:2 Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.
> 1:3 Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika.

Tazama namna uumbaji ulivyokuja kwenye Neno, ambaye alikuwa "hapo mwanzo". Kutokana na hili pekee tunaweza kuona kuwa maneno "hapo mwanzo" hayawezi kurejelea kwenye uumbaji. Inaweza tu kurejelea kwenye Neno, ambaye kupitia yeye vitu vyote viliumbwa. Na Neno ni nani? Mstari wa 14 unafunua juu ya hilo:

> Yohana 1:14 Naye **Neno** alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa **Mwana pekee atokaye kwa Baba**, amejaa neema na kweli.

Kwa mwanafunzi muaminifu wa Biblia, hili lipo wazi kabisa. Wanaoamini kwenye utatu pia wanalijua hili, na kwa hiyo wanajaribu mbinu nyingine. Wanadai kuwa neno "Naye" si neno mahsusi la kubainisha, kwa kuwa siyo sehemu ya maandishi ya awali. Kwa hiyo, kulingana na wanao amini kwenye utatu, "mwanzo" si mwanzo, kwa sababu neno "Naye" halipo. Wanajua kuwa ikiwa "mwanzo" unarejelea kwa Kristo, ingepingana na nadharia yao ya umilele wa watu watatu walio pamoja.

Inashangaza, wanaoamini kwenye utatu wanajipinga wao wenyewe bila ya kujali. Kwenye mistari minne inayofuatia, neno "Naye" halipatikani kwenye maandishi ya awali. Lakini ni nani atakayekataa kuwa kwenye vifungu hivi vinne, mwanzo halisi unarejelewa? Je, hakukuwa na mwanzo Mungu alipowaumba Adamu na Hawa?

> Mathayo 19:4 ...yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke,

Vipi kuhusu matetemeko ya ardhi, njaa, ugonjwa wa tauni, na vita ambavyo vimesemwa kwenye Mathayo 24; matukio haya hayana mwanzo? Bila shaka yana mwanzo. Yesu mwenyewe anasema hivi:

> Mathayo 24:8 Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu.

Je, tangu mwanzo wa huduma yake Yesu hakujua kuhusu Yuda?

> Yohana 6:64 ...Kwa maana Yesu alijua tangu mwanzo ni nani wasioamini, naye ni nani atakayemsaliti."

Je, hapakuwa na mwanzo wa mpango mbaya wa Shetani kuua? Ni kweli kabisa, kwa kuwa Shetani alianza maisha yake akiwa ni malaika mtakatifu!

> Yohana 8:44 ...Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo;...

Kwenye vifungu vyote vinne, neno "Naye" halipo kwenye maandiko ya asili. Bado wote watakubali kuwa neno "mwanzo" linaashiria mah-

ali halisi pa kuanzia kwa matukio yaliyoelezwa. Zaidi ya hayo, tazama namna Strong's Concordance inavyolifafanua neno 'mwanzo':

> kutoka G756; mwanzo, au (kwa hakika) yenye ukuu (kwenye matumizi mbalimbali ya utaratibu, wakati, mahali, au cheo):—mwanzo...

Ikitoa maoni yake juu ya Yohana 1:1, Thayer's Greek Lexicon inalifafanua neno 'mwanzo' kama:

> chanzo, asili; a. Limetumika hasa, la mwanzo wa vitu vyote:

Kwa uwazi, neno "mwanzo" linamrejelea Yesu; "hapo mwanzo kulikuwako Neno". Hata hivyo, wale wanaoamini utatu watabishana kuwa Neno lilikuwa ni Mungu, na Mungu hana mwanzo. Hii ni kweli. Hata hivyo, zingatia tafsiri sahihi ya Yohana 1:1:

*en 1722 arch 746 hn 2258 o 3588 logov 3056*
Hapo mwanzo Neno

*kai 2532 o 3588 logov 3056 hn 2258 prov 4314*
na Neno lilikuwa na

*ton 3588* yeon 2316 *kai 2532* yeov 2316 *hn 2258*
Mungu na Mungu alikuwa

*o 3588 logov 3056*
Neno.

Tazama namna neno "Mungu" (theos) kwenye Yohana 1:1 linavyoandikwa kwa njia tofauti kila wakati? Mara ya kwanza neno linatumiwa, ni nomino. Inarejelea kwa Mungu Baba. Mara ya pili neno linapotumiwa, ni kivumishi. Ina maana ya kuwa Neno lilikuwa la Uungu, au ni sawa na Mungu.

Tazama tafsiri ifuatayo ya James Moffatt, Hugh J. Schonfield na Edgar Goodspeed:

> ...na Neno lilikuwa ni takatifu.

*Today's English Version* inasomeka hivi:

> ...na alikuwa sawa na Mungu.

*The Revised English Bible* inasomeka hivi:

> ...na Mungu alivyokuwa, Neno alikuwa.

Zaidi ya yote, fikiria namna EJ Wagoner anavyoielezea Yohana 1:1:

> Neno lilikuwepo 'hapo mwanzo.' Akili ya mwanadamu haiwezi kufahamu enzi ambazo zimesambazwa kwenye kifungu cha maneno. Wanadamu hawajafumbuliwa kujua ni lini au ni jinsi gani Mwana alizaliwa;

Vile vile, kutoka kwa Uriah Smith, tunaambiwa hivi:

> Mungu peke yake ndiye asiye na mwanzo, kwenye enzi ya kwanza kabisa ambapo mwanzo ungeweza kuwepo, kipindi cha mbali sana ambacho kimsingi kwa akili zenye ukomo ni za umilele, Neno lilionekana 'Hapo mwanzo kulikuwako Neno. **naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu**.' Yohana 1:1.

Yohana 1:1 siyo tukio la kwanza ambapo tunaambiwa kuwa Mwana wa Uungu wa Mungu alikuwa na mwanzo. Ona jinsi ambavyo Ellen White anasema kuhusu Mithali sura ya 8:

> Na Mwana wa Mungu anasema hivi kumhusu Yeye mwenyewe: "**BWANA alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake**, kabla ya matendo yake ya kale. Nalitukuka tokea milele....Alipoiagiza misingi ya nchi; ndipo nilipokuwa pamoja naye, kama stadi wa kazi; nikawa furaha yake kila siku; nikifurahi daima mbele zake;" Mithali 8:22-30. (Patriachs and Prophets 34.1)

Enyi marafiki, ni Kristo ambaye anazungumza kwenye Mithali 8:22, na anasema kuwa: “BWANA alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake.” Kifungu kinaendelea kusema kuwa hii ilitokea "kabla ya matendo yake ya kale" (uumbaji). Hiki ndicho hasa ambacho Yohana 1:1-3 inakifundisha. Kwenye Yohana 1:1, “mwanzo” (wa Neno) inarejelea kwenye wakati wa kabla ya uumbaji wote.

Inafurahisha, Mathayo sura ya 1 na Luka sura ya 3 kila moja inaeleza nasaba ya ubinadamu wa Yesu. Sura zote mbili zinajumuisha vizazi vingi. Kwenye Yohana 1:1, tunapata nasaba ya Uungu wa Kristo. Kwenye suala hili, mtume aliuhitaji mstari mmoja tu: "hapo mwanzo kulikuwako Neno". Wakati fulani kabla ya uumbaji, Mungu Baba alimzaa Mwana. Kristo mwenyewe anakuambia: “**BWANA alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake**, kabla ya matendo yake ya kale.” (Mithali 8:22).

Zaidi ya hayo, Mika 5:2 inaelezea hivi: Kutokea kwa Kristo ni “tangu zamani za kale”; tangu milele. Kwa hivyo, Neno—mwana pekee wa Baba—lililetwa kutoka kwenye siku za kabla ya uumbaji; hata kabla ya wakati kuwepo. Ndiyo maana hauwezi kuhesabiwa na akili za wanadamu. Juu ya hili, Ellen White anasema:

> Kristo anawaonyesha kuwa, ingawa wanaweza kuhesabu maisha yake kuwa chini ya miaka hamsini, lakini maisha yake ya Uungu hayawezi kuhesabiwa kwa hesabu ya kibinadamu. Kuwepo kwa Kristo kabla ya kupata mwili wake hakupimwi kwa takwimu. (Signs of the Times, Mei 3, 1899)

Hekima ya Mungu ni ya ajabu kama nini! Mstari ule ambao wanaoamini kwenye utatu wanautumia kufundisha utatu wa utatu wa milele unafunza waziwazi kuwa Neno—Mwana wa Mungu—alikuwa na mwanzo! Na Yohana 1:14 inatufunulia kabisa Neno ni nani:

> Yohana 1:14 Naye **Neno** alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa **Mwana pekee atokaye kwa Baba**; amejaa neema na kweli.

Hili jambo likiwa akilini, Yohana 1:1 inaweza kusomeka kwa urahisi kwa

namna hii: "hapo mwanzo kulikuwako [mwana pekee wa Baba]". Ni ukweli ulioje ambao umetukuka!

## ISAYA 9:6

> Isaya 9:6 Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani.

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Kristo anaitwa "Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele". Hii inamaanisha utatu wa nafsi tatu za milele.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Unabii wa Isaya 9:6 unatabiri upendo wa Mungu kwa kumtoa Mwanawe kwa ajili ya ulimwengu. Pia, unaeleza huduma ya Kristo; maisha Yake, mafundisho, na miujiza. Hakuna sehemu ya mstari huu inayoonyesha mungu wa utatu.

Kama mtu anautafsiri mstari huu akimaanisha kuwa Kristo ndiye "Baba wa Milele", ni Mwana yupi ambaye amepewa mpaka aitwe hivi? Kufundisha kuwa Kristo ni Baba na Mwana ni Unitariani na sio Kuamini kwenye Utatu. Haya mafundisho yote siyo sahihi.

Kwa bahati mbaya, kamwe Yesu hajaitwa jina lolote kati ya majina haya kwenye Agano Jipya. Hivi ni vyeo vinavyoelezea maisha, huduma, na tabia Yake. Neno la Kiebrania la 'jina' ni 'shem' (H8034). Kwenye Thayer's Greek Lexicon kuna ufafanuzi wa hivi:

> jina, kama alama au ukumbusho wa umoja; kwa maana ya heshima, **mamlaka, tabia**:

Zingatia jina la "Ajabu" kama lilivyotajwa kwenye Isaya 9:6. Neno hili linarejelea hasa kwa mtu ambaye angefanya mambo ya ajabu, kama vile kutenda miujiza. Kwenye huduma Yake yote, ni kweli Yesu aliitimiza maana ya neno hili.

Sasa fikiria jina la "Mshauri". Kwenye maisha na huduma Yake, Yesu alikuwa ni mwalimu mkuu, mshauri, na mfariji ambaye ulimwengu umewahi kumfahamu. Kuhusu neno, "Mungu mwenye nguvu", hebu tuone jinsi ambavyo mtume Luka anavyomuelezea Yesu:

> Luka 9:43 Wote wakashangaa, **wakiuona ukuu wa Mungu.** Nao walipokuwa wakiyastaajabia mambo yote aliyoyafanya, aliwaambia wanafunzi wake,...

Neno la “Mfalme wa Amani” lilitimizwa kikamilifu kupitia maisha ya Kristo, hasa kwa kifo na ufufuo Wake. Mtume Paulo anaandika hivi:

> Waefeso 2:14 Kwa maana **yeye ndiye amani yetu**, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga;

Na vipi kuhusu neno: “Baba wa milele”? Tunajua kuwa Adamu ndiye baba wa wanadamu. Lakini Yesu anaitwa “Adamu wa mwisho” (1 Wakorintho 15:45-49). Kwa hakika, Kristo anafaa kuitwa “Baba wa milele,” si kwa sababu Yeye ni Mungu Baba, bali kwa sababu Yeye ni Adamu wa pili, na hivyo ni Baba mpya wa watoto wa Mungu waliozaliwa mara ya pili:

> 1 Wakorintho 15:22 Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.

Enyi marafiki, mtu anawezaje kutumia Isaya 9:6 kufundisha kuhusu utatu wakati mstari yenyewe unaanza kwa kusema: “Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume”? Mtu anayeamini kwenye utatu hata haamini kuwa Mungu alikuwa na Mwana wa kumtoa! Bila shaka, Isaya 9:6 ni Yohana 3:16 ya Agano la Kale. Kupitia unabii wa injili, Mungu anasema kuwa: “Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa” (Isaya 9:6). Na kwenye kuitangaza injili ya milele, Yesu anayarudia maneno hayo hayo:

> Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee...

## ISAYA 44:6

> Isaya 44:6 BWANA, Mfalme wa Israeli, Mkombozi wake, BWANA wa majeshi, asema hivi Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu.

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Kwenye Isaya 44:6, mzungumzaji Anajiita "mkombozi" na kisha anasema "zaidi yangu mimi hapana Mungu". Kwa kuwa Yesu ni Mkombozi wetu, ni lazima awe Mungu mmoja wa kweli.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Isaya 44:6 haisemi chochote kuhusu mungu wa utatu. Kujifunza kwa makini mstari huu pamoja na vifungu vingine vinavyohusika kwenye Isaya kutafunua wazi kuwa ni Mungu Baba ambaye anazungumza kwenye Isaya 44:6. Hili linaendana kikamilifu na maneno ya Yesu kwenye Yohana 17:3: "Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli".

Ni muhimu kutambua kuwa kuna mtu mmoja tu anayezungumza kwenye mstari huu, siyo wawili. Hivi ndivyo mstari ulivyosomeka kwa usahihi: "BWANA, Mfalme wa Israeli…BWANA wa majeshi".

Zaidi ya hayo, kwa sababu tu neno la "mkombozi" limetumika kwenye Isaya 44:6, hiyo haimaanishi moja kwa moja kuwa inarejelea kwa Kristo. Pia, Baba anaitwa Mkombozi. Kwenye Isaya 63:8, Baba anaitwa "Mwokozi". Na kwenye Isaya 63:9 tunaambiwa kuwa ni Baba ambaye "aliwakomboa" Israeli. Tunaweza kuwa na uhakika juu ya jambo hilo, kwa kuwa kwenye huo huo mstari, Mwana anatajwa kuwa ni "malaika wa kuwako Kwake". Sasa, angalia mstari wa 16 wa sura hiyo hiyo:

> Isaya 63:16 Maana wewe ndiwe baba yetu, ijapokuwa Ibrahimu hatujui, wala Israeli hatukiri, **wewe BWANA ndiwe Baba yetu, mkombozi wetu** tangu milele ndilo jina lako.

Acheni tuichunguze Isaya 49:7 pia. Kwa hapa, Mungu Baba anazungumza na anajiita "Mkombozi wa Israeli". Hatimaye, mtu hawezi kuitumia Isaya 44:6 kwa Kristo kwa dhana tu ya kwamba Anaitwa Mkom-

bozi, kwa vile tumeona hivi punde kuwa cheo hiki kinamhusu Mungu Baba pia.

Zaidi ya hayo, mzungumzaji anasema kuwa: "hakuna Mungu pembeni yangu". Hili pekee linawaondoa wale wengine wawili wanaodhaniwa kuwa washiriki wa utatu wa milele, wenye usawa! Sasa, angalia mstari wa 8 wa hiyo hiyo sura. Swali linaulizwa:

> Isaya 44:8 ...je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine.

Kwenye huu mstari, ni wazi kuwa mtu mmoja anazungumza, na kwamba mzungumzaji anajitofautisha Mwenyewe (Mungu mmoja wa kweli) dhidi ya safu kubwa ya miungu ya kipagani. Hiki ndicho kiini cha kifungu chote. Kwamba kuna Mungu mmoja wa kweli wa Israeli, tofauti na wingi wa miungu iliyopo katika mataifa ya kipagani. Tazama mstari wa 24:

> Isaya 44:24 BWANA, mkombozi wako, yeye aliyekuumba tumboni, asema hivi; Mimi ni BWANA, nifanyaye vitu vyote; nizitandaye mbingu **peke yangu**; nienezaye nchi; ni nani aliye **pamoja nami**?

Ni kwa nini mzungumzaji anasema kuwa Yeye aliziumba mbingu na Ardhi "peke yangu"? Kama inavyofunuliwa kwenye Waebrania 1:2 na Waefeso 3:9, "Mungu aliviumba vitu vyote kwa njia ya Yesu Kristo". Kwa hakika, Baba ndiye muanzilishi wa uhai wote. Yeye ndiye "ambaye vitu vyote vimetoka kwake". Sasa fikiria Ufunuo 4:11:

> Ufunuo 4:11 Umestahili Wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa.

Anayeabudiwa juu mbinguni kama Muumba wa vitu vyote ni Baba, kwa kuwa hata Kristo aliupokea uzima wake kutoka kwa Baba (Yohana 5:26). Ni Baba ambaye ameketi kwenye kiti cha enzi kwenye Ufunuo 4:11. Ni Baba anayepokea sifa: "Ee BWANA wa majeshi, Mungu wa

Israel, ukaaye juu ya makerubi, wewe, naam, wewe peke yako ndiwe Mungu wa falme zote za dunia, Wewe ndiwe uliyeziumba mbingu na nchi" (Isaya 37:16).

Kwenye 1 Wakorintho 15:28 tunasoma hivi:

> 1 Wakorintho 15:28 Basi, vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake, ndipo Mwana mwenyewe naye atatiishwa chini yake yeye aliyemtiishia vitu vyote, ili kwamba Mungu awe yote katika wote.

## ISAYA 48:16

> Isaya 48:16 Nikaribieni, sikieni haya; tokea mwanzo sikunena kwa siri; tangu yalipokuwapo, mimi nipo; na sasa Bwana MUNGU amenituma, na Roho yake.

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Kristo anasema kuwa: "Bwana MUNGU amenituma, **na** Roho yake". Kwa hiyo, Mungu na Roho ni watu tofauti.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Kristo anasema kuwa: "Bwana MUNGU amenituma, **na** Roho yake". Kama inavyothibitishwa na kiwakilishi "yake", Roho ni Roho wa Mungu; ni yake.

Fikiria namna Isaya 48:16 inavyosomeka kwenye tafsiri nyinginezo:

> Na sasa Bwana Mwenye Enzi Kuu amenituma mimi, **pamoja na** Roho wake.
> *New International Version*
>
> ...na sasa Bwana MUNGU amenituma mimi, **na** Roho wake.
> *American Standard Version*
>
> ...na sasa Bwana Mungu amenituma, **na kunipa** roho yake.
> *Bible in Basic English*
>
> ...na sasa Adonai ELOHIM amenituma mimi **na** Roho wake.
> *Complete Jewish Bible*
>
> ... na sasa Bwana Mungu amenituma, **na** roho yake.
> *Douay Version*
>
> ...Na sasa Bwana MUNGU amenituma mimi, **na** Roho wake.
> *English Standard Version*
>
> ...na sasa Bwana MUNGU amenituma mimi, **na** Roho wake.
> *Hebrew Names Version*

> ...Na sasa Bwana MUNGU amenituma mimi, **na** Roho wake.
> *New American Standard*
>
> ...Sasa, Bwana Mungu amenituma **pamoja na** Roho wake.
> *New Century Version*
>
> ...Na sasa Bwana Mungu amenituma mimi **na** roho yake.
> *New Revised Standard*
>
> ...Na sasa Bwana MUNGU amenituma mimi **na** Roho wake.
> *Revised Standard Version*
>
> ...Na sasa Bwana MUNGU amenituma, **nikiwa nimejazwa** Roho wake.
> *Today's New International Version*

Kila tafsiri ya Biblia inasema kuwa Mungu alimtuma Roho wake binafsi pamoja na Yesu duniani. Kwa hiyo, si Roho—kama nafsi ya tatu—aliyemtuma Yesu kwetu, bali ni Mungu Baba pekee aliyemtuma Kristo, "aliyejaliwa na Roho wake" (TNIV). Hili linadhihirishwa kwa wingi kupitia kitabu cha Isaya:

> Isaya 42:1 Tazama mtumishi wangu **nimtegemezaye**; mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye; **Nimetia roho yangu juu yake**; naye atawatolea mataifa hukumu.
>
> Isaya 11:2 **Na roho ya BWANA atakaa juu yake**, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha BWANA;
>
> Isaya 61:1 **Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu**; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.

Jambo lililosemwa na Baba kwenye Isaya 42:1, na kurudiwa na nabii kwenye vifungu vinavyofuatia, ni jambo lile lile linaloletwa kwenye Isaya 48:16: "Bwana MUNGU amenituma, na Roho yake". Yesu alitumwa na Baba pamoja na Roho Mtakatifu wa Baba. Hivyo, tunasoma kuwa: "Na roho ya BWANA atakaa juu yake". Isaya 11:2.

Kwenye Luka 4:18, tunaona utimilifu wa unabii wa Isaya:

> Luka 4:18 **Roho wa Bwana yu juu yangu**, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa,

## MSAIDIZI MWINGINE

> Yohana 14:16 Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Yesu anasema kuwa Msaidizi **mwingine** ataletwa. Kwa hiyo, ni lazima Msaidizi (Roho Mtakatifu) awe ni mtu tofauti na wa milele.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Yesu anasema kuwa: "Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu". Msaidizi (Roho Mtakatifu) ni Roho wa Kristo Mwenyewe. Anaitwa "mwingine" kwa sababu Yesu asingekuwa Msaidizi tena akiwa kwenye umbo la kimwili, la kibinadamu (ambalo wanafunzi walilijua) bali Msaidizi kwa Roho Wake.

Wanaoamini utatu wanakataa wazi wazi kuwa Roho Mtakatifu ni Roho wa Baba na Mwana. Kwenye kitabu chake, *Understanding the Trinity*, Mchungaji Max Hatton anasema hivi:

> Roho Mtakatifu anachukua nafasi ya Yesu…Yeye ndiye Mshauri wa Yohana 14:16.
>
> Roho Mtakatifu ni Nafsi ya Utatu; Yeye si Baba, wala si Mwana. Yeye ni Mmoja wa wale watatu ambao ni wa milele.

Vile vile, kwa mzungumzaji wa Kiadventista, Tony Rykers, Msaidizi wa Yohana 14 ni kiumbe mwingine wa Kimungu, aliyejitenga na Yesu. Anasema kuwa:

> Ni wazi kuwa Yesu ndiye Msaidizi wa kwanza. Endapo Roho Mtakatifu ni Mfariji mwingine, inamfanya awe sawa na Kristo, kwa hiyo ni kiumbe cha uungu, Msaidizi mwingine ambaye ataongoza na kumuongoza kila mmoja wetu.

Kinyume chake, Ellen White anatoa maoni yake juu ya Yohana 14:16, na kwa upinzani wa kipekee kwenye msimamo wa utatu, anasema kuwa:

> Hii inarejelea kwenye uwepo wa Roho wa Kristo kila mahali, aitwaye Mfariji. (14MR 179.2)

Kwenye sehemu nyingine pia anaandika hivi:

> Mwokozi ni Mfariji wetu. (8MR 49.3)
>
> Yesu Mfariji. (19MR 297.3)
>
> Acha wakisome sura ya kumi na saba ya Yohana, na wajifunze jinsi ya kuomba na jinsi ya kuishi kwenye maombi ya Kristo. **Yeye ndiye Mfariji**. (RH, Januari 27, 1903 aya ya 13)

Ingawa wale wanaoamini utatu wanabisha kuwa Roho Mtakatifu ni mtu mwingine, Ellen White anathibitisha kuwa Roho Mtakatifu ni Roho wa Kristo Mwenyewe:

> Anaivutia Mioyo—**Bwana Yesu amesimama kando**, akitembea nao, ndiye mfanyakazi mkuu. Endapo tunamtambua Kristo kama Yule ambaye yupo pamoja nasi kuandaa njia, **Roho Mtakatifu kando yetu** atayafanya yale yanayohitajika. (Manual for Canvassers, aya ya 40, 1902)

Akisisitiza kwa dhati umuhimu wa ukweli huu, Ellen White anaandika hivi:

> Sababu ya makanisa kuwa dhaifu na yenye ugonjwa yakiwa tayari kufa, ni kwa kuwa adui ameleta mvutano wa asili ambao unakatisha tamaa juu ya roho zinazotetemeka. **Amejaribu kufunga Yesu kwenye mawazo yao asionekane kama Mfariji**... (RH Agosti 26, 1890)

Ni adui anayedai kuwa Roho Mtakatifu ni nafsi ya tatu ya umilele wa pamoja. Ni adui anayetafuta kumfunga Yesu asionekane kuwa ni Mfariji. Je, Yesu anasema nini?

> Yohana 14:18 Sitawaacha ninyi yatima; **naja kwenu**.

Je, unakumbuka wanafunzi walimuuliza nini Yesu mara baada ya kuyasema maneno haya?

> Yohana 14:22 Yuda (siye Iskariote), akamwambia, Bwana, **imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu**, wala si kwa ulimwengu?

Jibu la Kristo lilikuwa ni hili:

> Yohana 14:23 …Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake.

Baada ya ukweli huu, wanafunzi walisimama imara sana. Kwenye *The Great Controversy*, tunasoma juu ya maagizo ya mwisho ya Mwokozi kwa wanafunzi Wake, pamoja na furaha yao kwenye kupata uwepo binafsi wa Kristo wa Siku ya Pentekoste.

> "Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili," akaongezea, "na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote," (Marko 16:15; Mathayo 28:20); wakati wa Siku ya Pentekoste **Mfariji aliyetajwa alishuka** na nguvu kutoka juu ikatolewa na **roho za wanaoamini zikasisimka walipofahamu kuwa Bwana wao aliyepaa yupo**... (GC 350.1)

Kujidhihirisha kwa Roho Mtakatifu ambako kulipokelewa na wanafunzi kwenye Siku ya Pentekoste kulikuwa ni pale "walipofahamu kuwa Bwana wao aliyepaa yupo"! Ni baraka iliyoje kusoma maneno ya mwisho ya Kristo: "na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:20). Wanafunzi walielewa kuwa Yesu alikuwa ni Msaidizi wao. Kwa kweli, walifurahia sana kuwa Yesu angali pamoja nao, nao walipata mvua ya mapema. Wale wanaoipokea mvua ya masika wataamini ukweli ule ule kama walivyoamini wanafunzi wa kwanza. Wataamini kuwa Kristo ndiye Msaidizi wao.

## WA AINA YAKE, MMOJA WA KIPEKEE

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Neno la Kigiriki la 'mzaliwa' ni 'monogenes'. Inarejelea kwa Kristo kuwa ni wa pekee au wa aina yake, na si kama Mwana halisi aliyezaliwa.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Neno 'monogenes' limetumika mara tisa kwenye Agano Jipya na kila mara, linarejelea kwa mzazi na mtoto. Siku zote neno linatafsiriwa kama 'mzaliwa' kwenye KJV, na kamwe kama 'pekee', au 'maalum'.

'Monogenes' ni neno linalotumika kwenye kila sehemu ya aya tano zinazofuatia. Kwenye kila hali, inarejelea kwa Yesu kuwa Mwana pekee wa Mungu.

> Yohana 1:14 Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee *[monogenes]* atokaye kwa Baba;
>
> Yohana 1:18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote; Mungu Mwana pekee *[monogenes]* aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.
>
> Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee *[monogenes]*, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.
>
> Yohana 3:18 Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu *[monogenes]*.
>
> 1 Yohana 4:9 Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee *[monogenes]* ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye.

Sababu ya kwa nini neno 'monogenes' limekuwa na utata sana ni kwa sababu wanaoamini kwenye utatu hawawezi kukubali kuwa Kristo

ndiye Mwana pekee wa Mungu. Hawawezi kukubali ufafanuzi wake ambao ni rahisi—mzaliwa pekee—kwa sababu unafunua kuwa Yesu alizaliwa, na kwa hiyo alikuwa na mwanzo. Kwa maana hii, wanadai kuwa 'monogenes' inamaanisha 'pekee' au 'wa aina yake', bila kujali nusu ya pili ya neno hilo kabisa. Fikiria jinsi neno la Kigiriki linavyofafanuliwa kwenye *Strong's Concordance*.

Monogenes (G3439) ni mchanganyiko wa maneno mawili ya Kigiriki:

> G3441 na G1096; mzaliwa pekee yaani wa kipekee.:- pekee (mzaliwa, mtoto)

Sehemu ya kwanza ya neno ni 'monos':

> Monos – 3441
> Wa pekee, mmoja, pekee.

Sehemu ya pili ya neno ni 'ginomai':

> Ginomai - 1096
> Kuzalisha - kuzaliwa, kutokea.

Kwa hiyo, 'monogenes' inaweza kutafsiriwa kama 'inayozalishwa kwa upekee'. Hii ndiyo sababu *Strong's Concordance* inafafanua kwa usahihi neno 'monogenes' kama "mwana wa pekee". *The New American Standard Bible* (NASB) pia inafafanua kuwa 'monogenes' ni kama "mwana wa pekee".

Kulingana na NAS Exhaustive Concordance, sehemu ya pili ya neno 'monogenes' ni 'genos' (G1085). 'Genos' maana yake ni 'kuzaliwa' au 'mwana'. Na mzizi wa neno 'genos' (G1085) ni 'ginomai' (G1096), ambalo tayari tumeona maana yake ni kuzalisha, kuzaliwa, au kutokea.

Kwa hivyo, bila ya kujali kama mtu anatumia KJV au NASB, tafsiri zote mbili zinaitafsiri 'monogenes' kama "mzaliwa wa pekee". Na zote mbili, *Strong's Concordance* na *NAS Exhaustive Concordance* zinaifafanua sehemu ya pili ya neno kuwa ama 'ginomai' (G1096) au 'genos' (G1085)

zote kwa pamoja. Maneno haya yanamaanisha "kutokea" na "kuzaliwa".

Kwa ushahidi zaidi, fikiria namna ambavyo neno 'genos' linavyotumika kwenye Matendo 18:24 na Matendo 17:28-29. Neno limetafsiriwa kama 'kuzaliwa' na 'mwana' kwa mpangilio huo. Kwa hivyo, mtu anaweza kutafsiri kwa usahihi 'genos' kama 'uzao wa kuzaliwa'. Na kwa kuzingatia sehemu ya kwanza ya neno ('mono'), hivyo ndivyo hasa Yohana 3:16 inavyosomwa kwenye KJV na NASB. Kwa kweli Mungu alimtuma "mwanawe pekee" ulimwenguni.

Kwenye kitabu cha Waebrania, tunapata neno lingine la Kigiriki ambalo limetumika kwa ajili ya Yesu. Neno hili ni 'gennao' (G1080), ambalo linamaanisha: "kuzaa, kuzalisha, kujifungua, kubeba mimba". Fikiria matumizi yake kwenye Waebrania 1:5:

> Waebrania 1:5 ...Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa [gennao]?...

Hapa tunapata neno la pili—nje ya 'monogenes'—ambalo linamaanisha 'mzaliwa. ', 'kuzalisha', na 'kujifungua'. Inafurahisha kuona kile kifungu cha Agano la Kale ambacho Paulo anakinukuu kutoka kwenye huu mstari. Hakika, mtume anarejelea waziwazi kwenye Zaburi 2:7, ambapo Daudi anatumia neno la Kiebrania la 'yalad'. 'Yalad' (H3205) inamaanisha "kuzaa, kuzaliwa, kuzalisha, kujifungua, utungu". Angalia mstari wa hapa chini:

> Zaburi 2:7 Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa [yalad].

'Genos', 'yalad', na 'gennao' yote yanamaanisha kitu kimoja: kuzaliwa. Kwenye Kiebrania na Kigiriki, kwenye Agano la Kale na Jipya, Mungu anasema kuwa ana "Mwanawe pekee"!

Hebu sasa turudi kwenye Waebrania sura ya 1:

> Waebrania 1:6 Hata tena, amletapo **mzaliwa wa kwanza** *[pro-*

*totokos]* ulimwenguni, asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu.

Hapa tunalipata neno lingine la Kigiriki linalotafsiriwa kama "mzaliwa wa kwanza" na linavyohusiana na Yesu Kristo. Ni 'prototokos' (G4416). Kutoka kwenye Thayer's Greek-English Lexicon, twasoma ya kuwa:

> Kristo anaitwa, **mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote, ambaye alikuja kupitia kwa Mungu kabla ya ulimwengu wote wa vitu vilivyoumbwa.**

Yohana 16 inaliangazia neno lingine ambalo linamtambulisha Kristo kama Mwana wa pekee wa Mungu. Hapa, Yesu anazungumza na wanafunzi Wake, na Anataja matendo mawili ambayo yametokea: kuja kwake "kutoka kwa Baba" na kuja kwake "ulimwenguni":

> Yohana 16:27 Kwa maana Baba mwenyewe awapenda kwa kuwa ninyi mmenipenda mimi, na kusadiki ya kwamba mimi nalitoka kwa Baba.
> 16:28 Nalitoka kwa Baba, nami nimekuja hapa ulimwenguni; tena nauacha ulimwengu; na kwenda kwa Baba.

Yesu anawaambia wanafunzi waziwazi kuwa alitoka (exerkomai) kutoka kwa Baba. Angalia jinsi wanafunzi wanavyouitikia ukweli huu. Wanatumia neno lile lile la Kiyunani:

> Yohana 16:30 ...twasadiki ya kwamba ulitoka kwa Mungu.

Baada ya kukiri kwa wanafunzi, Yesu anaomba kwa Baba kwa niaba yao. Kwenye maombi yake, Yesu anathibitisha kuwa wanafunzi wamepokea ushuhuda Wake, na kwa hakika wanaamini kuwa alitoka (exerkomai) kwa Mungu:

> Yohana 17:8 Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea, wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.

Matendo mawili ambayo Yesu anayaelezea kwenye Yohana 17 yana maneno na maana tofauti. Hata hivyo kwa kila moja ya maneno: "nalitoka kwa Mungu", "nalitoka kwa Baba", "kutoka kwa Mungu", na "nalitoka kwako", neno lile lile la Kiyunani linatumika. Neno hilo ni 'exerchomai' (G1831), na linamaanisha kuwa:

> kutoa (kihalisi au kwa njia ya mfano): - kuja-(mbele, nje), kuondoka (kutoka), kutoroka, kutoka nje, kwenda (nje ya nchi, mbali, nje; toka, toka huko), endelea (toka), sambaa nje.

*Thayer's Greek English Lexicon* inaifafanua 'exerchomai' kama "**kutoka kimwili, kutokea, kuzaliwa na**". Kinyume chake, neno linalotumika Kristo anaposema hivi: “Nami…nimekuja hapa ulimwenguni”, ni 'erchomai' (G2064), ambayo ina maana kwa urahisi: “kutoka sehemu moja hadi nyingine”. Kwa hiyo, Kristo anaposema kuwa: “Nilitoka [exerchomai] kutoka kwa Baba”, hasemi kuwa Alitumwa kutoka kwa Mungu, kama kwenye 'erkomai', bali anasema kuwa Yeye alitoka Kwake kihalisi; ya kuwa alizaliwa na Baba!

Mpaka hapa, tumeona maneno sita tofauti kwenye Kiebrania na Kigiriki ambayo yote yanamaanisha kuzaliwa, na yote yanatumika kwenye muktadha wa Yesu Kristo. Monogenes, genos, yalad, gennao, prototokos, na exerkomai. Sasa, acheni tuchunguze tafsiri ya Kiaramu.

Bila shaka, Biblia ya Peshitta ndiyo tafsiri bora zaidi ya Biblia iliyo karibu na The King James, ikitafsiriwa kutoka kwenye hati za Kiaramu na za Kisiria. Peshitta inaitafsiri Yohana 1:14 kwa "utukufu kama wa **Mwana pekee** atokaye kwa Baba;" na Yohana 1:18 kama "**mzaliwa wa kwanza** wa Mungu". Kwenye Yohana 3:16, 18 na 1 Yohana 4:9, vile vile inatumia neno la “**Mwanawe pekee**”.

Sasa, angalia uthabiti kwenye vifungu hivi vilivyoandikwa na Paulo na Yohana, kila kimoja kinapoandika kuwa Yesu ndiye Mwana pekee wa Mungu:

> Waebrania 1:6 Hata tena, amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni,...

> 1 Yohana 4:9 Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni,...

Kwa kuupinga ukweli huu moja kwa moja, mchungaji anayeamini kwenye utatu, Max Hatton anasema kuwa:

> Yesu alifanyika Mwana wa Mungu wakati wa kuzaliwa kwake kama mwanadamu. …

Je, ni nini tumekisoma hivi punde kwenye Waebrania 1:6?

> Waebrania 1:6 **Amletapo** mzaliwa wa kwanza ulimwenguni.

> 1 Yohana 4:9 Mungu **amemtuma** Mwanawe pekee ulimwenguni.

Yesu hakuwa mwana wakati wa kuzaliwa Kwake mwanadamu. Alikuwa ni Mwana kabla hata ulimwengu haujaumbwa! Ndiyo maana Anasema kuwa "Nalitoka [exerkomai] kwa Mungu" (Yohana 8:42). Ni kwa sababu hii ikawa Kristo "amefanyika bora kupita malaika, kwa kadiri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao" (Waebrania 1:4).

Yesu alipata jina bora zaidi kuliko malaika kwa sababu alirithi asili ya Uungu ya Baba yake tangu anazaliwa. Ila kwenye Waebrania 2:9-16, tunasoma kuhusu Yesu kufanywa awe "aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika" alipochukua asili yetu ya kibinadamu ambayo imetenda dhambi ("uzao wa Ibrahimu") huko Bethlehemu:

> Waebrania 2:9 ila twamona Yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika,...ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu.
> 2:14 Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo,...
> 2:16 Maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu.

Waebrania 2 inarejelea kwenye ubinadamu wa Kristo. Alishiriki damu na mwili wetu, akafanywa mdogo kuliko malaika kwa ajili yake.

Kinyume chake, kwenye sura ya 1—ambayo inarejelea Uungu wa Kristo—Paulo asema kuwa Yeye "amefanyika bora" kupita malaika. Kristo "amefanyika bora kupita malaika" kwa sababu Anabeba asili ya Uungu ya Baba yake ambayo Aliirithi tangu alipozaliwa. Waebrania 1 yote inahusu Uungu wa Kristo kama Mwana pekee wa Mungu.

Kumbuka tulichojifunza kuhusu neno 'yalad' lililotumiwa kwenye Zaburi 2:7. Neno hili linamaanisha kuzaliwa. Sasa tazama namna Paulo anavyolitafsiri neno hili kwenye lugha ya Kiyunani kwenye Agano Jipya. Paulo analitafsiri kwa usahihi neno 'yalad' kama 'gennao', ambalo kama tulivyoona linamaanisha kuzaliwa:

> Waebrania 1:5 Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wowote, ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa *[gennao]*? Na tena, Mimi nitakuwa kwake Baba, na yeye atakuwa kwangu Mwana?

Kwenye mstari ambao unafuatia, Paulo anatufunulia kuwa Kristo alikuwa ni Mwana kabla hajaja kwenye ulimwengu huu:

> Waebrania 1:6 Hata tena, amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni, asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu.

Wakati akiinukuu Zaburi 2:7, Paulo anauliza hivi: BWANA aliniambia, "Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa"? Ukweli ni kuwa maneno hayo ni ya Yesu pekee. Hakuna malaika anayeitwa mzaliwa wa Baba, na kwa hiyo, Yesu amefanyika "bora kupita malaika" (Waebrania 1: 4)!

Tafadhali usilitafsiri vibaya hili jambo kumaanisha kuwa Mwana aliumbwa. Tazama namna EJ Wagoner anavyolifafanua jambo hili kwenye kitabu chake cha *Christ and His Righteousness*:

> Maandiko yanasema kuwa Kristo ndiye "mwana pekee wa Mungu." **Amezaliwa, hajaumbwa**.

Kwenye Waebrania 1:6, Kristo anaitwa "mzaliwa wa kwanza" (prototokos) kabla ya kuzaliwa Kwake huko Bethlehemu. Kwenye Wae-

brania 1:4, Paulo anaandika kuwa Kristo “amefanyika [ginomai] bora kupita malaika”. Tayari tumeona kuwa hii inarejelea kwenye kuzaliwa Kwake kwenye umilele, na sio kule Bethlehemu, kwa kuwa huko Bethlehemu alifanywa "mdogo punde kuliko malaika". Ila tazama namna ambavyo neno hilo hilo linavyotumika kwenye kurejelea kuzaliwa kwa Kristo kwa uhalisia huko Bethlehemu:

> Wagalatia 4:4 Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa *[ginomai]* na mwanamke, amezaliwa [ginomai] chini ya sheria,

Ni wazi kuwa, neno “amezaliwa na mwanamke” linamaanisha kuzaliwa kwa Yesu kama mwanadamu. Hata hivyo, hili ni neno lile lile la Kiyunani (ginomai) ambalo linatumika kwenye Waebrania 1:4. Ina maana: "kuja kwenye uwepo, kuanza kuwa, kupokea kuwa". Kwa hiyo, tunaposoma kwenye Waebrania 1:4 kuwa Yesu amefanyika (ginomai) bora kupita malaika, hii lazima irejelee kwenye kuzaliwa Kwake halisi kwenye umilele. Ndiyo maana Paulo anaendelea kusema kwenye mstari wa 6 kuwa: Baba “amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni”. Mpaka hapo, tunaweza kuwa na uhakika kuwa Yesu alikuwa ni Mwana mzaliwa wa Mungu kabla ya ulimwengu kuumbwa. Ni uhusiano ambao ni halisi, sio wa kufananisha.

Kila kifungu kwenye Biblia kinachohusu uhusiano wa Baba na Mwana hakina pendekezo kuwa kinapaswa kueleweka kwa njia ya sitiari. Badala yake, kila kifungu kinarejelea kwenye upendo wa Mungu kwa kutupatia Mwana wake wa pekee. Hata hivyo, wanaoamini kwenye utatu hufanya kiini hasa cha injili iwe ni sitiari—bila kibali chochote cha kufanya hivyo—na hivyo kuharibu nguvu zake!

Kwa mfano, inapozungumza kuhusu Yakobo na Yohana, Biblia inawaita “wana wa ngurumo”. Marko 3:17. Je, radi iliipiga ardhi na kuwazaa Yakobo na Yohana? Hapana. Neno hilo ni la mfano wa wazi wazi; waliowekwa ili kuonesha tabia zao za ujeuri na bidii. Hata hivyo hakuna lugha kama hiyo inayotumika wakati wowote kurejelea kwa Baba na Mwana. Kinyume chake, kila mstari unaohusika na uhusiano wao umebeba neno kutoka kwenye lugha ya Kiyunani au Kiebrania ambayo in-

amaanisha kuzaliwa au kutoka, kama tulivyoona.

Zaidi ya hayo, kwa kukataa kuwa Yesu amezaliwa kweli, unaupunguza udhihirisho mkuu wa upendo wa Baba kwa wanadamu. Kama vile 1 Yohana 4:9 inavyosema, "Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye." Zaidi ya hayo, kwenye Luka 12:9, Yesu asema hivi: "na mwenye kunikana mbele ya watu, huyo atakanwa mbele ya malaika wa Mungu."

Enyi marafiki, fundisho la utatu limejengwa juu ya ukanusho kama huu. Mchungaji Max Hatton anaandika hivi:

> Maneno ya Baba na Mwana yanapohusiana na Yesu hayawezi kuwa ni halisi...Uhusiano wa Baba na Mwana kwenye Uungu unapaswa kueleweka kwa maana ya sitiari, si kwa maana halisi.

Kauli hii inapopingwa zaidi, Yesu anatusihi kwa kusema:

> Luka 12:8 Nami nawaambia, kila atakayenikiri mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkiri yeye mbele ya malaika wa Mungu;
>
> Ufunuo 3:5 ...Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake.

Wengine wanasema kuwa huu mjadala wa kuhusu uana halisi wa Kristo siyo wa muhimu. Lakini angalia namna ambavyo huu ni wa muhimu milele yote:

> Luka 12:9 na mwenye kunikana mbele ya watu, huyo atakanwa mbele ya malaika wa Mungu.

Enyi marafiki, uzima wetu wa milele upo hatarini. Ni wale tu wanaokiri jina la Kristo kuwa Mwana pekee wa Mungu wataipata ahadi yake: "atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima" (Ufunuo 3:5).

## MZALIWA WA KWANZA

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* 'Mzaliwa wa kwanza' maana yake ni 'aliyechaguliwa' au 'aliyetangulia'. Haimaanishi kuzaliwa kwa maana halisi.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* 'Mzaliwa wa kwanza' [prototokos G4416] imenukuliwa mara tisa kwenye Agano Jipya. Imetafsiriwa mara saba kama 'mzaliwa wa kwanza', na mara mbili kama 'wa kwanza kuzaliwa'. Yafikirie matumizi yake kwenye Wakolosai 1:15:

> Wakolosai 1:15 naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, **mzaliwa wa kwanza** *[prototokos G4416]* wa viumbe vyote.

Sasa, tazama namna ambavyo Paulo anavyolitumia neno lile lile (prototokos) kwenye Waebrania 1:6:

> Waebrania 1:6 Hata tena, amletapo **mzaliwa wa kwanza** *[prototokos G4416]* ulimwenguni, asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu.

Kutoka kwenye *Thayer's Greek-English Lexicon*, twasoma ya kuwa:

> Kristo anaitwa, **mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote, ambaye alikuja kwetu kupitia Mungu kabla ya ulimwengu mzima wa vitu vilivyoumbwa.**

Tukio la kwanza ambalo neno 'mzaliwa wa kwanza' linaonekana kwenye Biblia ni kwenye Kutoka sura ya 12:

> Kutoka 12:12 Maana nitapita kati ya nchi ya Misri usiku huo, nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa mwanadamu na wa mnyama; nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri; Mimi ndimi BWANA.

Bila shaka, neno la 'mzaliwa wa kwanza' linapaswa kutolewa kihalisi kwenye suala hili. "Wazaliwa wa kwanza wote kwenye nchi ya Misri,

wa mwanadamu na wa mnyama” walipigwa usiku huo. Ila ukombozi ulifanywa kwa wazaliwa wa kwanza wa Israeli. Je, kuna mtu wa kusema kuwa aya ifuatayo ni ya mfano pia?

> Kutoka 13:13 Kila **mzaliwa wa kwanza** wa punda utamkomboa kwa mwanakondoo; na kwamba hutaki kumkomboa, utamvunja shingo; **na kila mzaliwa wa kwanza wa binadamu katika wanao utamkomboa.**
> 13:15 basi ilikuwa hapo Farao alipojifanya kuwa mgumu ili asitupe ruhusa kuondoka, BWANA akawapiga **wazaliwa wa kwanza** wote waliokuwa katika nchi ya Misri, wa binadamu na wa mnyama; kwa ajili ya hayo namtolea BWANA wote wafunguao tumbo, wakiwa waume; lakini **wazaliwa wa kwanza wote wa wana wangu nawakomboa.**

Wakfu halisi ni kuwekwa wakfu kwa “mzaliwa wa kwanza wa binadamu katika wanao”. Ilikuwa ni sherehe iliyofanyika kwa Israeli ili kuhakikisha kwamba kamwe hawatasahau jinsi ambavyo Mungu aliwaongoza kutokea Misri. Kama ujumbe ambao ulipaswa kupita kwenye kila kizazi, sasa Israeli angeweza kuwakomboa watoto wake, kwa kuwa Mungu alikuwa amesha wakomboa kutoka Misri. Alikuwa amewapata tena.

Neno 'mzaliwa wa kwanza', kama lilivyotumiwa kwenye kurejelea kwa Kristo, halimaanishi mteule, au ambaye ni mashuhuri zaidi. Neno la Mungu halitumii neno hilo kama tamathali ya usemi. Kama ilivyowekwa wakfu kwa wazaliwa wa kwanza wa Israeli, ilikuwa ni kuwekwa wakfu kwa Mzaliwa wa Kwanza wa Baba.

## UBATIZO WA KRISTO

*Vipingamizi vya wanaoamini utatu:* Baba anazungumza kutokea mbinguni, Yesu Kristo anasimama ndani ya maji, na Roho Mtakatifu anashuka kwa namna ya njiwa. Hapa kuna utatu wa nafsi tatu za milele.

*Majibu ya Uthibitisho wa Biblia:* Ni utukufu wa Mungu, Roho wa Mungu, anayeshuka wakati wa ubatizo wa Yesu. Hili hasa ndilo linalofafanuliwa kwenye Yohana 15:26.

> Yohana 15:26 Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, **huyo Roho wa kweli, atokaye kwa Baba**, yeye atanishuhudia.

Roho wa kweli (Roho Mtakatifu) "kutoka kwa Baba". Nini maana ya "kutoka kwa"? Inamaanisha "**kutoka**". Ni neno lile lile ambalo limetumika kwenye Mathayo 4:4 na Luka 4:22.

> Mathayo 4:4 Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno **litokalo** katika kinywa cha Mungu.

> Luka 4:22 Wakamshuhudia wote, wakiyastaajabia maneno ya neema **yaliyotoka** kinywani mwake, wakasema, Huyu siye mwana wa Yusufu?

Roho anayeshuka akiwa kwenye umbo kama la njiwa anatoka kwa Baba. Ni Roho wa Baba. Ndiyo maana Ellen White anasema hivi: "moja kwa moja **kutoka kwenye kiti cha enzi** akiutoa utukufu wake mkuu". Fikiria kauli hii inayofuatia kutoka kwenye The Desire of Ages, ambapo Ellen White anaonyesha uwezo wa Roho Mtakatifu kwenye maisha ya Kikristo:

> Ni kusudi lake kuwe na ushawishi wa juu zaidi kwenye ulimwengu, **unaotoka kwenye chanzo cha nguvu zote**, utakuwa ni wao. (The Desire of Ages, 679.3)

Nguvu hii inatokea wapi? "Inatoka", "inaibuka", na "hutoka" kutoka kwa

Mungu. Na kwa kuwa Kristo ni Mwana wa Mungu, Roho wa Uungu pia hutoka Kwake:

> Roho Mtakatifu, **anayetoka** kwa Mwana pekee wa Mungu… (The Review and Herald, Aprili 5, 1906 aya ya 16)

Je, Roho Mtakatifu ni nani? Ni Roho wa Mungu na Kristo:

> Warumi 8:9 Lakini ikiwa **Roho wa Mungu** anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata Roho, Lakini mtu awaye yote asipokuwa na **Roho wa Kristo**, huyo si wake.
>
> Yohana 14:23 Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda, **nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake.**

## UAMUZI BINAFSI

Mpendwa Msomaji,

Tumechunguza kila kifungu kikuu kwenye Biblia ambacho kinatumiwa katika kufundisha kuhusu utatu wa nafsi tatu za milele. Lakini hakuna hata moja ya vifungu hivi vinavyothibitisha ufafanuzi wa aina hiyo. Kinyume chake, tumeona kuwa ukweli kuhusu Baba, Mwana wake wa pekee, na Roho Mtakatifu wao unaweza kufundishwa wazi wazi kutoka kwenye vifungu vivi hivi!

Zaidi ya hayo, maneno, 'utatu', 'mungu mwana', na 'mungu roho' hayajaandikwa hata mara moja kwenye Biblia. Uwe makini na hoja hii.

Wanaoamini utatu hawana mstari hata mmoja kwenye Maandiko yote ili kufundisha kuwa Mungu ni umoja wa nafsi tatu za milele. Ila kama ambavyo tumeona hivi punde, Maandiko yapo wazi sana kwenye kufundisha kuwa Baba ndiye "Mungu wa pekee wa kweli", kuwa Yesu "kweli" ni "Mwanawe pekee", na kuwa Roho Mtakatifu ni "Roho wa Mungu" na "Roho wa Kristo".

Kwenye msalaba wa Kalvari, Yohana 3:16 ilitimizwa. Hapa ndipo Mungu alipomtoa Mwanawe wa pekee. Cha kufurahisha, kulikuwa na matabaka mawili ya watu pale msalabani siku hiyo. Wengi walikuwa wakimdhihaki Kristo, wakisema: “jiokoe nafsi yako; ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani” (Mathayo 27:40). Lakini katikati ya dharau na dhihaka za umati ule, sauti ya askari wa kipagani ilisikika. Kwa imani, alisema kuwa: “Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu” (Mathayo 27:54).

Askari huyu aliikiri imani yake, na akaokolewa kwa sababu hiyo. Ingawa makuhani, watawala, na wanatheolojia waliodai kuwa na ujuzi mwingi wa Neno la Mungu walijiamulia hatima yao kwa ajili ya hukumu ya milele. Cha kusikitisha ni kuwa wale walio wengi waliifuata njia ya watu hao wanaodaiwa kuwa ni wenye hekima.

Tuje kwetu sisi watu wa leo, wito siyo kitu cha tofauti na hilo. Yohana

3:16 inamtaka kila mmoja aufuate msimamo wake.

Je, wewe utamuunga mkono askari huyo mnyenyekevu na kusema ya kuwa: “Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu”? Au utawafuata wale wanaojiita walimu wetu nyakati hizi, ambao kwa mara nyingine tena wanakana kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu aliye hai?

Kama ilivyokuwa kwa askari wa kipagani na makuhani wa Kiyahudi, uamuzi wako pia utaamua hatima yako ya milele.

www.earthenvessels.org.au
info@earthenvessels.org.au

***Je, Mungu na Kristo wana uhusiano halisi wa Baba na Mwana? Au ni sitiari?***

Kwa uwazi na unyenyekevu,
Bill Pinto anachunguza Biblia
ili kuamua mara moja na kwa wote:
Je, Mungu ni Utatu?

Nusu ya mwisho ya kitabu hiki ina
majibu kwa pingamizi 15 za
kawaida kuhusu ukweli kuhusu Baba,
Mwanawe wa pekee, na Roho Mtakatifu.

EARTHEN VESSELS
2 CORINTHIANS 4:7